

UK. 22

**MBAPPÉ AIKERA BAYERN MUNICH**


# Nipashe

Jumanne Juni 11, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581704

MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.ippmedia.com
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper


# Washauri diaspora waruhusiwe kupiga kura

UKURASA 2




Brenda Kifanga



Suriama Hassan

**Wataalamu** waeleza tatizo la kupoteza kumbukumbu

UKURASA 3



**Ajali** ilivyoua watatu, wakiwamo mashuhuda

UKURASA 4



**Baraza** laingilia kati kupanda bei ya vocha

UKURASA 4



Mke wa aliyekuwa mfanyabiashara maarufu mjini Moshi Evagro Msele, Beatrice Kwayu (36), akiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi mkoani Kilimanjaro kwa shtaka la mauaji ya mumewe yaliyotokea Mei 25, mwaka huu, Pumuani A, Kata ya Kirua Vunjo nyumbani kwa mzazi mwenzake. **PICHA: MARY MOSHA**

# Anayedaiwa kuua mume apandishwa kizimbani

UK. 3

UKURASA WA 5

## SERIKALI YADAIWA BIL. 1/- HUDUMA, MAKANDARASI

HADI kufikia Machi 2024, serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya Sh. bilioni 1.03 ya madeni yaliyohakikiwa ya wazabuni wa bidhaa na huduma pamoja na makandarasi.



UKURASA WA 24

## SIMBA, YANGA KUKUTANA NGAO YA JAMII AGOSTI

# Uzazi wa mpango kwa wanaume wabuniwa

UKURASA 2

**MICHEZO** STARS KUSAKA POINTI TATU KWA ZAMBIA UK.24

**KATUNI** UK.6



Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi, Jaji Jacob Mwambegele, akifungua mkutano wa Tume na viongozi wa taasisi za dini, uliofanyika ukumbi wa Mlimani City jijini Dar es Salaam jana. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa Uchaguzi, Kailima Ramadhani. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wapendekeza diaspora waruhusiwe kupiga kura

**Na Halfani Chusi**

ASASI za kiraia zimependekeza kuwapo na mabadiliko ya sheria ili Watanzania wanaoishi nje ya nchi (diaspora) na wakimbizi waruhusiwe kupiga kura katika uchaguzi mkuu na uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kwenye mkutano baina ya Tume Huru ya Uchaguzi (NEC) na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, Mwakilishi wa taasisi inayoshughulikia wakimbizi nchini ya Diginity Kwanza, Brenda Kifanga, alisema pia kuna umuhimu wa kuwaangalia wakimbizi waliokaa nchini muda mrefu au kuzaliwa, wapewe uraia ili nao waweze kupiga kura.

Alisema Katiba inasema ukiwa na uraia zaidi ya mmoja (uraia pacha) huwezi kupiga kura, na kutaka kundi hilo lihusishwe katika mikutano ili wajue haki zinazowahusu na kuelewa kwanini hawaruhusiwi kupiga kura.

Alisema kitendo hicho kitafanya idadi ya wapiga kura iongezeke na kuongeza amani na upendo miongoni mwa Watanzania, na kusisitiza kuwa marekebisho ya sheria hayaepukiki.

Aidha, alisema kundi la wakimbizi halina tofauti na diaspora ambao pia Katiba haiwaruhusu kupiga kura, na kwamba mabadiliko ya sheria yakifanyika kila Mtanzania atakuwa na haki ya kuchagua kiongozi anayemtaka.

Mwakilishi kutoka Taasisi ya TOSUCADO, Suriama Hassani, alishauri elimu iendelee kutolewa zaidi akidai wengi bado wana dhana potofu kwamba hata akijiandikisha kwenda kupiga kura wanaoshinda ni walewale.

Alisema kitendo hicho kinafanya wengine wapoteze imani ya kuchagua au kujiandikisha katika daftari la wapigakura.

Ramadhani Msele kutoka Taasisi inayojihusisha na Watu Waliotengwa (PDF), alishukuru NEC kwa kukutana na asasi za kiraia kwa ajili ya kupigana msasa kuhusiana na taratibu za uchaguzi, na kwamba utasaidia kuongeza uelewa na kushawishi wengi kujiandikisha.

Akifungua mkutano huo, Mwenyekiti wa NEC, Jaji Jacobs Mwambegele, alisema maandalizi ya daftari la kudumu la wapiga kura unajumuisha uhakiki wa vituo vya kupigia kura, uboreshaji wa majaribio, ununuzi wa vifaa na ushirikishwaji wa wadau.

Alisema tayari Tume imeanza mchakato wa uboreshaji wa daftari na unatarajiwa kuzinduliwa rasmi mkoani Kigoma, Julai mosi mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa.

Alisema ibara ya 74(6) ya Katiba imeipa tume jukumu la kusimamia na kuratibu uandikishwaji wa wapigakura kwa ajili ya uchaguzi wa Rais Wabunge na Madiwani.

Alisema uboreshaji huo kama ilivyokuwa katika uchaguzi uliopita utahusisha matumizi ya teknolojia ya Biometric Voters Registration (BVR) ambayo inatumika katika kumtambua mtu na kumtofautisha na mwingine.

"Pia utahusisha uchukuaji wa alama za vidole vya mikono, picha na saini na kuzihifadhi kwenye kanzidata ya wapigakura.

"Wakati wa zoezi hilo, tume imeweka utaratibu kwa watu wenye ulemavu, wazee, wagonjwa, wajawazito, na wenye watoto wachanga watapewa fursa ya kuhudumiwa bila kupanga foleni," alisema Jaji Mwambegele.

Aidha, aliwataka wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura ili waweze kupata nafasi ya kupiga kura na kuchagua kiongozi wanayemtaka.

"Ninapenda kuwahimiza katika majukwaa yenu, niwaombe asasi za kiraia kwa umoja wenu kuwaelimisha na kuwahamasisha wananchi kuendelea kuzingatia sheria za uchaguzi, kanuni za uboreshaji maelekezo ya tume na kwa upande wetu tume tutazingatia katiba, sheria za uchaguzi na kanuni zilizotungwa chini ya sheria katika zoezi la uboreshaji.

"Kama mnavyokumbuka mwaka jana tume ilifanya uboreshaji wa majaribio katika kata ya Ikoma iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Rorya mkoani Mara na Kata ya Ng'ambo iliyoko Halmashauri ya Manispaa Tabora, lengo la majaribio hayo yalikuwa ni kupima uwezo wa vifaa na mifumo ya uandikishaji itakayotumika wakati wa uboreshaji wa daftari," alisema Jaji Mwambegele.

Alisema katika kuendana na mabadiliko ya teknolojia, ili kurahisisha kazi hiyo tume imeboresha mfumo wa uandikishaji ambao kwa mara ya kwanza utamwezesha mpigakura aliyeko katika daftari kuboresha taarifa zake au kuhama kituo kwa kutumia simu au kompyuta na baadaye kutembelea katika kituo anachokusudia kujiandikisha ili apatiwe kadi yake ya mpigakura.

Wiki iliyopita Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Watanzania waishio Korea alisema serikali ipo katika hatua za mwisho za kubadili sheria ya ardhi na uhamiaji ili kutoa hadhi maalumu kwa diaspora.

Suala la diaspora limekuwa na mjadala mwingi tangu serikali zilizopita kilio kikubwa kikiwa haki ya uchaguzi, uwekezaji na uraia pacha hatua ambayo ililazimu serikali kuja na sera ya diaspora ambayo bado haijaruhusu kundi hilo kupiga kura.

Baadhi ya nchi za Afrika Mashariki ikiwamo Kenya imeruhusu diaspora kushiriki katika uchaguzi.

# Uzazi wa mpango kwa wanaume wabuniwa

**Na Mwandishi Wetu**

DAKTARI Bingwa wa Tiba ya Familia kutoka Hospitali ya Agakhan, Willbroad Kyejo, alisema ujio wa dawa ya uzazi wa mpango kwa wanaume ni hatua kubwa na inaweza kuwa na manufaa makubwa kwa jamii kwa kuzingatia changamoto za sasa za uzazi wa mpango.

Aidha, alisisitiza umuhimu wa kuwapo na mfumo mzuri wa kutoa elimu, usimamizi wa athari na kuhakikisha dawa hizo zinapatikana wakati wote zitakapohitajika na watumiaji.

Dk. Kyejo aliyasema hayo jana ikiwa ni siku tano tangu Shirika la Utangazaji la Marekani la CNN kuripoti kuwa watafiti kutoka Taasisi za Kitaifa za Afya na Baraza la Idadi ya Watu nchini Marekani wamefikia hatua nzuri kutengeneza dawa ya uzazi wa mpango kwa wanaume.

Dawa hiyo ambayo sasa ipo tayari kwa majaribio, wanaume hupaka kwenye mabega yao mara moja kwa siku ili kuzuia uzalishaji wa mbegu za kiume kwenye korodani na inaelezwa kufanya kazi kama ya wanawake.

Dk. Kyejo alisema kama dawa hizo zikianza kufanya kazi zinasaidia kuboresha uwiano wa majukumu kwa wanaume na wanawake kwa kuwa suala hilo limezoeleka kuwa ni jukumu la wanawake pekee.

"Kwa mujibu wa utafiti, jeli hii imeonyesha ufanisi mkubwa wa kupunguza uzalishaji wa mbegu za kiume kwa kiwango kinachoweza kuzuia mimba. Hii inatoa chaguo jingine la kuaminika kwa wanaume," alisema.

Alitaja faida nyingine kuwa mwanamume ana uwezo wa kupata mtoto kama akihitaji kwa kuwa matokeo ya utafiti huo yameonyesha kuwa endapo mwanamume ataacha kutumia jeli hiyo, uzalishaji wa mbegu za kiume unarudi kwenye hali ya kawaida ndani ya wiki nane hadi 10.

Aidha, alisema kama ilivyo kwa dawa nyingine za homoni, inaweza kuwa na athari kama vile mabadiliko ya hisia, ngozi kuwa kavu au yenye mafuta na hamu ya tendo la ndoa. Ni muhimu kwa watumiaji kuelewa na kufuatilia athari hizo.

Alisema pia kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania, upatikanaji wa dawa hizo unaweza kuwa changamoto. Ni muhimu kuwa na mikakati ya kuhakikisha zinapatikana kwa urahisi na kwa bei nafuu.

Alisema kwa kuwa hii ni teknolojia mpya, kutakuwa na haja ya kutoa elimu kwa jamii kuhusu matumizi sahihi na faida zake. Kampeni za uhamasishaji zinaweza kusaidia kuongeza uelewa na kupunguza unyanyapaa au upotoshaji wa taarifa.

Alishauri kuwapo mfumo mzuri wa kutoa elimu, usimamizi wa athari za upande na kuhakikisha kuwapo dawa za kutosha kwa wale wanaozihitaji ili kuboresha afya ya uzazi na kuboresha ubora wa maisha ya wanandoa.

CNN imeeleza kuwa Mkuu wa Tawi la Taasisi ya Kitaifa ya Afya ya Watoto na Maendeleo ya Binadamu ya NIH, Diana Blithe, alisema katika utafiti wa awali wa jeli hiyo iliyoitwa testosterone au placebo wanaume walipaka kila siku kwa wastani wa miezi 22.

Jeli hiyo inatumia mbinu sawa na vidonge vya kudhibiti uzazi kwa wanawake ya homoni mbili ambazo ni nestorone, progestion na testosterone zinazozuia ukuaji wa mbegu za kiume kwenye korodani.

Alisema watafiti wamekuwa wakitengeneza na kuboresha kipimo na mkusanyiko wa jeli tangu mwaka 2005, lakini jaribio la hivi karibuni lililojumuisha wanandoa zaidi ya 300 limefanikiwa.

Alisema kiwango cha kawaida cha mbegu za kiume ni kati ya milioni 15 hadi milioni 200 za mbegu kwa mililita ya shahawa, na tafiti zimeonyesha kuwa viwango vya mbegu za kiume chini ya milioni moja kwa mililita ni vya chini vya kutosha kuzuia mimba.

"Katika jaribio la kliniki asilimia 86 ya wanaume walifikia viwango hivi vya chini vya mbegu za kiume ndani ya wiki 15 za kutumia jeli. Kwa baadhi, ilifanya kazi hata haraka zaidi, ikizuia uzalishaji wa mbegu za kiume ndani ya wiki nne hadi nane," alisema.

CNN iliripoti kuwa Blithe alikataa kusema kama kulikuwa na mimba zisizotarajiwa wakati wa jaribio hilo akisisitiza kuwa watafiti wanatumaini kuwa na takwimu ya mwisho iliyochapishwa kwenye jarida la matibabu.

Alisema ikiwa mtumiaji wa mafuta hayo ataacha kwa siku mbili au zaidi homoni zake zitaanza kupona, lakini inachukua wiki nane hadi 10 kwa mbegu za kiume kurudi kwenye viwango ambavyo vinaweza kusababisha mimba.

Kwa mujibu wa CNN, Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO) lilijaribu kutengeneza sindano za uzazi wa mpango kwa wanaume zilizotumia mchanganyiko sawa wa homoni, mbinu iliyoonyesha kuwa na ufanisi, lakini usajili wa utafiti ulisimamishwa mwaka 2011, kwa sababu sindano zilisababisha athari nyingi za upande, ikiwa ni pamoja na unyogovu mkali.

Mmoja wa waliojaribu jeli hiyo, Matthew Trevino (35), kutoka Sacramento, California, alikuwa akipaka kwenye kila bega asubuhi na hajapata madhara makubwa zaidi ya kuongezeka uzito na hamu ya tendo la ndoa.

## HABARI KITAIFA

# Anayedaiwa kumuua mumewe apandishwa kizimbani

**Na Mary Mosha,**
MOSHI

BEATRICE Elias (36), mkazi wa Katanini, Kata ya Karanga katika Manispaa ya Moshi, amepandishwa kizimbani akikabiliwa na kesi ya mauaji ya kukusudia ya mume wake, Evagro Msele.

Msele (43) aliyekuwa mfanyabiashara maarufu katika mji wa Moshi, aliuawa Mei 25, mwaka huu kwa kuchomwa kisu mgongoni, akiwa nyumbani kwa mtu anayedaiwa kuwa mzazi mwenzie.

Mshtakiwa alifikishwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, Herieth Mhenga.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Hendry Daudi, alidai kuwa kesi hiyo namba 15731 ya mwaka 2024 inayomkabili Beatrice, upelelezi wake haujakamilika.

Msele, aliuawa Mei 25 mwaka huu, majira ya saa 3:50 usiku na mtu anayedaiwa kuwa mkewe wa ndoa, katika eneo la Pumuwani A, Kata ya Kirua Vunjo, Wilaya ya Moshi, baada ya kumkuta nyumbani kwa mwanamke mwingine.

Beatrice ameshtakiwa kwa kosa la mauaji, chini ya kifungu cha 196 na 197 cha Sheria ya Makosa ya Jinai, Sura 16 ya Sheria hiyo iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022.

Baada ya kusomwa maelezo hayo, mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote, kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza kesi hiyo.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 25, mwaka huu itakapotajwa tena mahakamani hapo.

# Mtaalamu aeleza tatizo kupoteza kumbukumbu

**Na Christina Mwakangale**

HIFADHI ya kumbukumbu ya muda mrefu na mfupi katika ubongo ina tatizo ikiwamo kuzongwa na msongo wa mawazo, 'karani' anayeshughulika kuhifadhi na kusambaza mafaili hayo hadi kwenye mfumo wa fahamu, atachanganya taarifa.

"Kwenye ubongo kuna sehemu tunaita 'file clerk' (karani wa mafaili), ni kama yule mtu ambaye tunamwambia kalete mafaili. Katika ubongo kuna mafaili mengi sana, ila kuna faili ambalo unaliambia nalihitaji hili faili sasa, karani kalibebe..."

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Damas Mlaki, amesema hayo akitoa mada kuelimisha umma kuhusu 'Uhusiano kati ya Kupoteza Kumbukumbu na Afya ya Akili'.

Akifafanua kuhusu aina nne za kumbukumbu katika ubongo, ikiwamo mfumo tumishi yaani karani, ambaye shughuli yake ni kupokea taarifa ya aina gani na faili linalohitajika wakati huo.

"Magonjwa ya akili yanaweza kumkumba mtu na kumsababishia kuchanganya mafaili yaliyohifadhiwa. Sayansi inaonesha kwamba yapo magonjwa ambayo unaweza ukapoteza kumbukumbu za matukio, lakini nyingine zisipotee sana.

"Ili taarifa ziweze kuhifadhiwa kwanza zinasajiliwa kama vile ilivyo masijala na ili usajili lazima milango ya fahamu mitano iwe inafanya kazi, kukiandikisha hicho kitu. Ili uandikishe lazima kiwe kimepelekwa katika eneo la kuhifadhi kumbukumbu za muda mrefu au mfupi.

> **"Kumbukumbu za muda mrefu, kuna sehemu za ubongo ambazo zinahusika. Kama eneo linahusika lina shida ambalo lina 'consolidate' (linaunganisha), ukapita muda unasahau," anasema Dk. Damas.**

"Kumbukumbu za muda mrefu, kuna sehemu za ubongo ambazo zinahusika. Kama eneo linahusika lina shida ambalo lina 'consolidate' (linaunganisha), ukapita muda unasahau," anasema Dk. Damas.

Anafafanua kila aina ya kumbukumbu ilivyo na umuhimu, kwa kuwa huhifadhi taarifa na endapo zinahitajika mfumo tumishi (karani), huzifuata katika masijala ya ubongo na kuchukua faili lenye taarifa hizo kwa ufahamu, akisema ni kitendo kinachochukua sekunde chache.

"Mwanasayansi mmoja kila alipokuwa anampa mbwa chakula aligonga kengele na mbwa anakuja huku akiwa anatokwa na udenda. Siku nyingine aligonga kengele, lakini chakula hakumwandalia...

"Mbwa alifikiri ile sauti ndio chakula, mbwa akaja vilevile na udenda, kufika chakula hamna. Maana yake, mbwa alipata hisia kwa kutumia kumbukumbu ya sauti ya kengele na kutokwa na udenda, bila kujali atakikuta chakula au la."

"Hata kama uliwahi kuadhibiwa hisia zinahifadhiwa, kwa hiyo ukifika au ukitaka kurudia kutenda kosa ambalo lilisababisha ukaadhibiwa hisia zinarudi, unasema hapana, huwezi kutenda tena," anasema bingwa huyo.

Bingwa mbobezi huyo anasema, ili binadamu awe na uwezo wa kukumbuka, ni lazima karani katika ubongo awe thabiti kwenye mfumo wa kurejea yaliyopita na yaliyohifadhiwa.

Anaeleza kwamba magonjwa yanayoathiri ubongo ni mengi na kumbukumbu za mtu, na kwamba kunahitajika uchunguzi na matibabu kulingana na aina ya kumbukumbu inayopotea.

"Matibabu yapo ya aina tofauti kama vile mlo kamili wenye virutubisho, kulala, ushauri wa kisaikolojia, kujisomea hadithi, kusoma kwenye mitandao ni kuupa mazoezi ubongo, unatulia unapata oksijeni na kumbukumbu kuongezeka," anasema Dk. Damas.

Dk. Damas ana angalizo kwamba waliothiriwa na magonjwa ya akili kama sonona, muda wa kupona ni chini ya miezi tisa hata kama hawajapewa matibabu, huku akitaja sababu ya kupona ubongo hujitibu kwa mfumo wake wenyewe au kwa kuanzishwa tiba na wataalamu mapema.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Ajali ilivyoua watatu, wakiwamo mashuhuda wawili

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

WATU watatu wamefariki duniani mkoani Manyara wakiwamo wawili waliokwenda kushuhudia ajali na mwingine aliyekuwa kwenye gari dogo kuruhusiwa kuendelea na safari.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi, George Katabazi, alisema ajali hiyo ilitokea Juni 9, mwaka huu majira ya saa 4:30 usiku katika barabara ya Singida-Babati katika mteremko wa Mogitu wilayani Hanang'.

Waliofariki ni wanaume wawili ambao walikuwa wanashuhudia ajali na mwanamke aliyekuwa dereva wa gari dogo, akisubiri magari yaruhusiwe kuondoka kuendelea na safari na kuparamiwa na basi, mali ya Kampuni ya Arusha Express na kufa hapo hapo.

Aidha, alisema gari lenye namba za usajili T914CAX Scania, iliigonga Scania yenye namba za usajili T1395A na iliyokuwa na namba T914CAX iliziba barabara na kukaa upande na kusababisha magari yasipite eneo hilo.

Katabazi alisema askari walifika eneo la tukio na kuanza kuruhusu magari ndipo gari la kampuni ya Arusha Express yenye namba za usajili T162 AGB lililokuwa likitokea Bukoba kwenda Arusha, dereva alishindwa kulimudu na kugonga Scania namba T914CAX, bodaboda na gari ndogo Toyota Mitsubishi na kugonga basi lililokuwa pembezoni mwa barabara.

Alisema majeruhi wa ajali hiyo ni watano akiwamo dereva wa kampuni ya Arusha Express iliyosababisha ajali na wote wako Hospitali ya Tumaini ya Wilaya ya Hanang' wakiendelea na matibabu.

Vilevile, alisema chanzo cha ajali ni dereva kushindwa kulimudu gari lake kwenye mteremko na aliposimamishwa na askari alikaidi.

Aliwashauri wananchi inapotokea ajali waangalie usalama wao kwanza na waepuke kwenda eneo la ajali.

Aidha, Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa ajali hiyo kwa kukagua mfumo wa breki kuona kama lilishindwa kufanya kazi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiongoza kikao cha ndani kuhusu Mradi wa Liganga na Mchuchuma kilichofanyika ukumbi wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Mlimwa jijini Dodoma jana. Kikao hicho kilihudhuriwa na Naibu Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Waziri wa Madini, Waziri wa Viwanda na Biashara, Waziri wa Mipango na Uwekezaji, Waziri wa Fedha, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baadhi ya makatibu wakuu na watalaamu. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Baraza laingilia kati kupanda bei vocha

**Na Jenifer Gilla**

SAKATA la kupanda kwa bei ya vocha za kukwangua limeifikia Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC), ambalo limewaagiza watoa huduma za mitandao kuwadhibiti mawakala wanaopandisha bei bila kufuata utaratibu.

Aidha, limewashauri kutoa taarifa kwa watumiaji kutonunua vocha hizo na kuweka utaratibu wa kutoa malalamiko wanapokutana na kadhia hiyo ili kukomesha tabia hiyo mapema.

Hali hiyo imekuja ikiwa ni takribani wiki mbili tangu bei ya bidhaa hiyo kupanda kutoka Sh. 500 hadi 600 na Sh. 1,000 ikiuzwa hadi Sh. 1,200 huku kwenye karatasi zikiwa zimeandikwa bei ya awali.

Taarifa kwa umma iliyotolewa na baraza hilo hivi karibuni ilieleza kuwa kumekuwa na malalamiko ya watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu kupanda kwa bei za vocha za simu za mkononi katika maeneo mbalimbali zikitofautiana baina ya wauzaji.

Kupitia taarifa hiyo, Katibu Mtendaji wa Baraza, Mary Msuya, alisema Baraza hilo lilipokea taarifa kupitia kamati za watumiaji za mikoa zikionyesha kuwa vocha ya Sh. 500 inauzwa kati ya Sh.550 hadi 600, Sh. 1,000 kuuzwa kati ya Sh. 1,100, hadi 1,200 kinyume na bei elekezi inayoonyeshwa kwenye vocha husika.

Alitaja mikoa ambayo Baraza limepokea malalamiko hayo kuwa ni Dar es Salaam, Rukwa, Iringa, Ruvuma, Manyara, Lindi, Mbeya, Mtwara na Songwe na linaendelea kufuatilia katika mikoa mingine kwa lengo la kupata taarifa zaidi ya bei hizo.

"Katika kushughulikia changamoto hiyo, Baraza limeshauriana na watoa huduma za mawasiliano ya simu kufuatilia mawakala wao na kupiga marufuku upandishaji holela wa bei za vocha," alisema Mary.

Baraza limeshauri watumiaji wa huduma za mawasiliano kununua vocha kwa kupitia simu zao za mkononi wakati changamoto hii ikitafutiwa ufumbuzi na kuendelea kutoa taarifa za kupanda bei kiholela katika maeneo mbalimbali ya nchi ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

**MADUKA MTAANI**

Huko mitaani bado baadhi ya maduka yanauza vocha za kukwangua kwa bei ya Sh. 1,100 hadi 1,200 na mengine yakilazimika kutouza hali inayowaweka watumiaji katika wakati mgumu.

Leonard Urassa ni mmoja wa wanaouza vocha ya Sh.1,000 kwa Sh. 1,100 akitoa sababu kuwa analazimika kuuza hivyo ili kupata faida yake ya awali kwa kuwa ameuziwa na wakala wa jumla Sh. 980 kutoka Sh. 950 iliyokuwapo mwanzo.

Alisema pia anauza vocha ya Sh. 500 kwa Sh. 550 kwa sababu na ameinunua Sh. 480 kutoka Sh. 430 huku akikiri kuwa hatonunua tena vocha za aina hiyo kwa sababu hata upatikanaji wa wateja kwa sasa umekuwa mgumu wengi kuhamia kwenye vocha za kurusha.

Naye Athnat John anasema tangu mawakala wapandishe bei za vocha hizo ameacha kuzinunua kwa kuepuka hasara.

Changamoto hiyo pia iliibuliwa bungeni Mei 29, mwaka huu na Mbunge wa Viti Maalum, Tunza Malapo, aliyehoji serikali ina mpango gani juu ya kupanda kwa bei za vocha za kukwangua.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Maryprisca Mahundi alisema wizara imewaagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kufuatilia suala hilo ili kuhakikisha kuwa watoa huduma za simu hawapandishi bei bila kufuata utaratibu.

# Ufuta tani 3,500 uliokwama wauzwa

**Na Julieth Mkireri,** KIBITI

TANI 3,500 za ufuta zilizokwama kuuzwa tangu Juni 6, mwaka huu kutokana na mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) kushindwa kufanya kazi zimeuzwa mwishoni mwa wiki katika Wilaya ya Kibiti, Mkoa wa Pwani.

Tani hizo zimeuzwa katika uzinduzi wa mnada wa zao la ufuta wa msimu wa mavuno ya mwaka 2024/2025 uliofanyika mwishoni mwa wiki.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi mjini Kibiti baada ya uzinduzi wa mnada huo, Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Pwani (CORECU), Mantawela Hamisi, alisema ufuta huo umeuzwa Sh. 3,653.21 kwa kilo.

Mantawela alisema Juni 6 ilitokea tatizo la kimfumo katika soko la bidhaa Tanzania na kusababisha ufuta huo kushindwa kuuzwa kwa siku ilivyopangwa na baada ya taratibu kufanyika mnada ulifanyika Juni 8, mwaka huu.

Aliwataka wakulima na viongozi wa vyama vya msingi vya kilimo AMCOS mkoani humo kuzingatia usafi wa zao hilo kabla ya kupeleka kwenye maghala.

Mwenyekiti wa CORECU, Mussa Mng'elesa aliwakumbusha wakulima wanaposafirisha mazao kuhakikisha wana nyaraka muhimu zinazotakiwa.

Mng'elesa pia amevielekeza vyama vya msingi vinapopokea mazao ya wakulima viwaeleze siku yatakapouzwa kwa njia ya mnada, huku akiwahakikishia wakulima kwamba pamoja na kikwazo cha barabara ufuta katika maeneo yote utakusanywa na kuuzwa kwenye minada.

Siku mbili kabla ya kufanyika mnada huo baadhi ya wakulima waliohudhuria uzinduzi wa mnada walisema kama suala la mfumo wa TMX halijakaa vizuri ni vema wakaendelea kutumia masanduku ili minada iende kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Kibiti, Kanal Joseph Kolombo, akiwa katika mnada huo wa uzinduzi ambao haukufanikiwa kufanyika kwa mara ya kwanza, alisema serikali haiko tayari kusikia suala la mkulima kucheleweshewa fedha zake baada ya mnada na badala yake kila mhusika anatakiwa kufuata taratibu.

HABARI KITAIFA

# EU kuendelea kuipiga jeki Tanzania nishati safi

**Na Joseph Mwendapole**

UMOJA wa Ulaya (EU), umeahidi kuendelea kufadhili miradi ya nishati safi ya kupikia kupitia mfuko maalumu wa nishati safi ili kuiwezesha Serikali ya Tanzania kufikia malengo yake.

Malengo ya serikali ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2034 asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia na kuachana na mkaa.

Hayo yalisemwa jana na Meneja Mradi wa Nishati kutoka Umoja wa Ulaya, Massimiliano Pedretti, kwenye mjadala wa wadau wa sekta ya nishati waliokutana kujadili na kutathmini uelekeo wa sekta ya nishati.

Wadau hao walikuwa wakijadili sekta hiyo ilipotoka, ilipo na inapoelekea baada ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2022/2023, changamoto na namna ya kukabiliana nazo.

Alisema watafanya hivyo kuunga mkono juhudi za serikali katika mkakati na utekelezaji kufikia azma ya asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ifikapo 2034.

Alisema ili Tanzania iweze kufikia azma yake ni lazima ichukue jitihada za kuweka mazingira mazuri kwa wauzaji wa mitungi ya gesi, watengenezaji wa majiko ya umeme ili kuchochea wananchi kutumia nishati safi ya kupikia kwa gharama nafuu na upatikanaji wa haraka.

Tayari mradi wa mfuko maalumu wa nishati safi ya kupikia unafanya kazi na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha taasisi kama Magereza, shule, hospitali kupitia Wakala wa Nishati REA wanafanya kazi kwa pamoja na kuweka miundombinu ya nishati safi ya kupikia kwenye maeneo yao.

Naye Meneja mradi wa matumizi bora ya umeme kutoka Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP), Aaron Cunningham, alisema UNDP iliamua kuunga mkono jitihada za Serikali ya Tanzania kwenye sekta ya nishati safi ya kupikia kwa kuhakikisha pia inaanzisha programu hiyo ili kuwe na matumizi bora ya nishati ya umeme kwenye vifaa vitakavyotumiwa na wadau.

Tayari wamesha ainisha viwango vitakavyotumiwa kwenye bidhaa aina tano kama vipoza umeme, jokofu, televisheni, feni na majiko ya umeme ili vitumie umeme kidogo.

Mradi huo unatekelezwa kwa pamoja na Wizara ya Nishati tangu walipoanzisha mwaka 2022 na wamekuwa bega kwa bega na Shirika la Viwango Tanzania TBS ili viwango hivyo vitoe unafuu wa matumizi ya umeme kwenye vifaa hivyo. Umoja wa Ulaya umekuwa ukichangia kwa kiasi kikubwa kwenye bajeti na miradi ya maendeleo hususani miradi ya umeme.

Wizara ya Nishati imewatoa hofu wadau wa sekta binafsi kuwa serikali inathamini mchango wa matumizi yote ya nishati safi ya kupikia ikiwamo umeme, gesi na nishati zingine zote ambazo ni rafiki kwa mazingira na afya.

Hayo yalisemwa kwenye mkutano huo na Kamishna Msaidizi wa Maendeleo ya Umeme wa wizara hiyo, Styden Rwebangila, aliyemwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba kwenye mjadala wa wadau hao wa sekta ya nishati.

"Napenda kuwatoa hofu wadau wa sekta binafsi na Watanzania kuwa nishati safi ya kupikia inajumuisha nishati zote na sio gesi pekee kama wengine wanavyodhani," alisema Kamishna Rwebangila.

Alisema Wizara ya Nishati inathamini mchango unaotolewa na wadau wa maendeleo hususani Umoja wa Ulaya kwa kufadhili miradi mbalimbali kwenye sekta ya nishati hususani nishati safi ya kupikia na itaendelea kushirikiana nao kwenye upangaji wa mipango mkakati na uendelezaji wa sera.

Mkutano huo uliohudhuriwa na taasisi zilizo chini ya Wizara ikiwamo REA, EWURA, TPDC, PURA, TANESCO pamoja na wadau wa maendeleo na sekta binafsi.



Mkurugenzi wa Kampuni ya Heroes Mining Camp, Basil Roman Njau (wa pili kushoto), akitoa msaada wa vyakula kwa yatima wa mji mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Serikali yadaiwa bil. 1/- huduma, makandarasi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HADI kufikia Machi 2024, serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya Sh. bilioni 1.03 ya madeni yaliyohakikiwa ya wazabuni wa bidhaa na huduma pamoja na makandarasi.

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema hayo jana bungeni wakati akijibu swali la Mbunge wa Masasi, Geofrey Mwambe (CCM), aliyetaka kujua ni kiasi gani hadi sasa serikali inadaiwa na wazabuni, wafanyabiashara, makandarasi na walipakodi kutokana na huduma, kazi na kodi zilizozidi.

Akijibu swali hilo, Dk. Mwigulu alisema hadi kufikia Machi 2024, serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya Sh. bilioni 1.03 ya madeni yaliyohakikiwa ya wazabuni wa bidhaa na huduma pamoja na makandarasi.

Alisema kati ya kiasi hicho Sh. bilioni 1.02 ni madeni ya wazabuni wa bidhaa na huduma na Sh. bilioni 8.75 madeni ya makandarasi.

"Hadi Machi 2024, serikali imeshalipa jumla ya Sh. bilioni 949.31 sawa na asilimia 92 ya madeni yaliyohakikiwa," alisema.

Pia alisema hadi kufikia Machi 2024, serikali ilikuwa inadaiwa jumla ya Sh. bilioni 80.06 ya madeni yaliyohakikiwa yanayotokana na kodi (VAT Refunds Claims).

"Hadi Machi 2024, serikali imefanya marejesho ya jumla ya Sh. bilioni 675.1 sawa na asilimia 96 ya lengo kwa kipindi hicho," alisema Dk. Nchemba.

Katika swali lake la nyongeza Mwambe, alihoji ni lini serikali itakuwa tayari kulipa madeni yote ya zabauni ambayo inadaiwa ili kuwaondolea usumbufu wazabuni wanaupata hivi sasa kutoka taasisi za kifedha.

Akijibu swali hilo Dk. Nchemba, alisema serikali imeweka mikakati ya kulipa madeni yote.

"Kwanza nipongeze serikali awamu ya sita kwa jitihada za kulipa madeni haya kwani yalikuwa ya muda mrefu, lakini katika kipindi hichi cha miaka mitatu ya serikali ya awamu ya sita kiasi kikubwa sana kimeshalipwa," alisema.

## CCM yafurahishwa uwekezaji viwanda nchini

**Na Steven William,** MUHEZA

CHAMA cha Mapinduzi kimesema serikali inafarijika inapowaona wazawa wanachukua hatua ya kuwekeza katika viwanda ili kupunguza gharama za kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Hayo yamesemwa juzi na Katibu wa CCM Taifa, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kutengeneza nyaya za umeme cha Tanga Cable kilichopo jijini Tanga.

Dk. Nchimbi alisema hakutakuwa na mafanikio ya kweli kama sekta binafsi haitashiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

"Tunapata faraja sana tunapoona wazawa Watanzania wanachukua hatua ya kuanzisha viwanda," alisema.

Dk. Nchimbi alisema kuna changamoto kubwa ya kuagiza bidhaa nje ya nchi na kwamba uanzishwaji wa viwanda hivyo utasaidia kupunguza changamoto hizo na kuongeza ajira kwa Watanzania.

Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Dk. Batilda Burian, alisema Mkoa wa Tanga ulikuwa unasifika kwa viwanda na mikakati ya mkoa ni kuhakikisha wanaongea na wamiliki wa viwanda vilivyokufa ili waweze kuvifufua na kuwasimamia wawekezaji wapya waendelee kuleta.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Zainab Abdallah, Mkurugenzi Halmashauri ya Muheza Dk. Jumaa Mhina, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Muheza Erasto Mhina, Mbunge wa Jimbo la Muheza, Hamis Mwinjuma na Katibu wa CCM wilaya hiyo, Simon Leng'ese kwa nyakati tofauti walisema kuwa katika wilaya ya Muheza ipo ardhi kubwa kwa wawekezaji kujenga viwanda na vijana wapate ajira.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wanaopoteza kumbukumbu wasinyanyapaliwe

**MWISHONI** mwa wiki wataalamu bingwa na bobezi wa magonjwa, afya ya akili na mfumo wa fahamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, wametoa ufafanuzi namna ubongo wa binadamu unavyofanya kazi na kuhifadhi kumbukumbu.

Ingawa wana angalizo kwamba wanaopoteza kumbukumbu, wanaweza kusababishiwa magonjwa ya akili kama vile msongo wa mawazo, lakini vilevile kupotea kwa kumbukumbu mbaya ni tiba ya asili ya kiungo hicho muhimu kwa mwili wa binadamu.

Akitoa mfano mtu anaposhuhudia mauaji ya kikatili huwa haitoki kwenye kumbukumbu yake na tiba itakayomfaa ni kupoteza kumbukumbu.

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu kutoka hospitali hiyo, Dk. Damas Mlaki, ametoa darasa hilo kwa umma, akisema jamii inapaswa kuzingatia elimu kuhusu afya ya akili, kwa manufaa ya ustawi wa jamii kwa ujumla.

Magonjwa yanayohusisha ubongo kutofanya kazi yake ipasavyo ni msongo wa mawazo pia kiharusi na waliojeruhiwa sehemu fulani ya ubongo kutokana na ajali na kukwamisha utendaji kazi wa ubongo ipasavyo.

Kadhalika, wapo ambao hupata athari hasa kupoteza kumbukumbu za masuala mbalimbali ambazo ubongo kwa mfumo wake thabiti, huzihifadhi kwa matumizi ya baadaye.

Msongo wa mawazo, sonona, watu kupitia na kuishi kwenye changamoto za maisha ambazo hazipati ufumbuzi wa mapema, huuathiri ubongo na kuhitaji kupewa matibabu ya dawa ama ushauri.

Mbinu za kujikinga na namna ya kufanya ubongo utunze kumbukumbu, inaelezwa kuwa ni kufanya mazoezi ya kimwili na kiakili, lishe bora na kupata usingizi wa kutosha usiopungua saa nane.

Inashauriwa watu kuzingatia usingizi ili kurejesha kumbukumbu na wanafunzi wanapewa angalizo la kutoa muda wa kujisomea kwa kuupumzisha ubongo kwa kupata usingizi jambo ambalo ni muhimu.

"Wanaokesha, wanafunzi kusoma bila kuupa nafasi usingizi ni tatizo. Wanaweza hata wanachokisoma wasikikumbuke katika chumba cha mtihani. Inahitaji ulale angalau saa nane kwa siku, ili kuzihuisha kumbukumbu."

Mbinu nyingine na kutunza kumbukumbu ni kuupa ubongo mazoezi ya kiakili, wataalamu wanasisitiza pia kuangalia filamu, kusoma vitabu, gazeti, kucheza michezo ya asili kama bao, kwa sababu mtu anatumia fikra ili kumshinda mwenziwe.

Wito wetu kwa watu wote ni jamii izingatie ushauri wa wataalamu wa afya, ili kuboresha ustawi kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Vilevile, jamii iache unyanyapaa kwa ambao uwezo wao wa ubongo na kutunza kumbukumbu ni duni hasa watoto, ambao wanapokuwa masomoni hushindwa kufikia wastani wa juu, kwa matamanio ya wazazi au walezi.

Mkurugenzi Mtendaji wa hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala, anasema jamii hasa familia, iache kufananisha uwezo wa ubongo baina ya mtoto mmoja na nduguze, kwani ni kawaida kutofautiana kutokana na ubongo ulivyoendelezwa.

Utafiti unaofanywa maeneo tofauti duniani unaonesha kuwa, uwezo wa ubongo kati ya binadamu mmoja na mwingine hutofautiana, licha ya kuwa pengine wana rika sawa hata kama watoto wa familia moja.

Jamii inatakiwa kuacha kusema vibaya mtoto mwenye uwezo mdogo hata kumnyanyapaa na ni vyema ubongo wa watoto hao ukaanza kuendelezwa mapema ili kukuza nafasi ya kutunza kumbukumbu za wanachojifunza hata kukuza vipaji vyao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






### Muungwana Lazima Nilonge

## Dharau kwenye zebra zinatuchosha

Na Joyce Lameck

**KUNA** mazoea ambayo sasa yamekithiri kwa madereva wengi kutokuheshimu alama za pundamilia ambazo ni vivuko vya wanaotembea na kusababisha ajali.

Kutoheshimu vivuko kwenye barabara kubwa na ndogo kumesababisha vifo na majeraha pia uharibifu wa mali. Wanaoathirika zaidi ni watoto, wanaoishi na ulemavu, wazee, wanaotumia vileo na hata wagonjwa.

Madereva wengi kuanzia wa bodaboda hadi malori kwenye miji mikubwa na midogo wanapokuwa barabarani hawaheshimu mistari ya pundamilia au zebra na kusababisha ajali, tena nyingine wakati mwingine zikizotokea jirani na kivuko.

Wanaoumia wanaingia kwenye hatari kwani wanaamini kuwa sehemu hiyo ni salama kutumiwa lakini sivyo, iwapo gari ndogo au basi la abiria linasimama, bodaboda huchomoka na kusababisha ajali. Tunajiuliza hivi bodaboda hawana ufahamu kuhusu kuheshimu vivuko hivyo?

Licha ya elimu ambazo zimekuwa zikitolewa mara kwa mara, kuhusu zebra kuna usumbufu kila wakati.

Kisheria zebra zinapaswa kuheshimiwa na watumiaji wote kuanzia madereva pamoja na wanaotembea kwa kufuata taratibu na kanuni zilizowekwa ili kuimarisha usalama pande zote.

Kwa upande mwingine, wanaotembea wanashauriwa kusimama na kuhakikisha kuwa magari yote yamesimama kabla ya kuingia kwenye kivuko cha pundamilia.

Sheria ya usalama barabarani inasema ni lazima dereva kuzingatia kuwa anapaswa kusimama mahali popote ambapo alama hiyo itakuwa imewekwa.

Pia kila anayetumia kivuko cha wanaotembea anatakiwa kuwa na tahadhari kubwa na pia akiangalia 'spidi' ahakikishe anatumia kivuko kuvuka barabara na si kwa mambo mengine.

Ni lazima madereva wajifunze kuwa itakapotokea anayetembea anatumia au anataka kukitumia, dereva wa gari atasimama kabla ya kivuko hicho ambacho hakiongozwi na taa za barabarani, ishara au askari.

Dereva akiwa amejiridhisha kuwa hakuna mtembea kwa miguu anayevuka au anayekusudia kuvuka barabara hiyo, inamsaidia kuepuka makosa kwani hakuna yeyote aliyekusudia kuvuka kwa wakati huo, hivyo anaweza kutembea kivukoni.

Halazimiki kusimama kila wakati ila, kama amejihakikishia kuwa hakuna anayevuka, dereva anatakiwa kupunguza mwendo na kuangalia na baada ya hapo ataendelea na safari.

Kwa hiyo dereva atasimama kwenye eneo kabla ya zebra pale wakati wote ambao atawaona waenda kwa miguu, wakiwa wanatembea pembezoni mwa kivuko na wakati mwingine wakiwa wanavuka kutoka upande mmoja kwenda upande wa pili wa barabara.

Kufanya hivyo ni lazima kwani baadhi ya madereva hawajali, hawazingatii sheria na kanuni za kiusalama kwao au kwa watu wengine na kusababisha kuongezeka ajali za barabarani.

Kwa mujibu wa sheria ya usalama barabarani ya mwaka 2002 sura ya 168 kifungu cha. 73(2) watumiaji wote wa barabara wanatakiwa kuheshimu na kufuata ishara zilizowekwa barabarani, ili kuepusha ajali zinazotokea kwa uzembe.

Kuna mambo muhimu ya kuzingatia unapokuwa katika eneo la zebra, kabla ya kuendelea na safari au kuvuka kutoka upande mmoja kwenda wa upande wa pili wa barabara ikiwa ni pamoja na kupunguza mwendo unapoikaribia zebra usiingie na kuizuia ili wanaovuka waione.

Lengo ni ili angalau uwe katika mwendo wa uwezekano wa kusimama, ikiwa kuna mtu atakuwa anavuka barabara au kutaka kuvuka barabara.

Sheria inawaelekeza madereva kuwa iwapo kuna mtu anasubiri kuvuka kwenye zebra, wasimame kumpisha avuke, wasimame kwanza ili avuke au aanze kuvuka, pia kama watamkuta katikati au anamalizia kuvuka waache amalize kuvuka.

Vile vile wasimpigie honi aliyesimama kupisha watu kuvuka kwenye kivuko, kadhalika wanaonywa wasimpite au kuovateki aliyesimama kupisha wanaovuka kwani kumpita kunaweza kusababisha ajali.

Aidha, amwashirie dereva mwenzie kusimama, iwapo anahisi amempuuza na anataka 'kuovateki' akiwa amepisha waotembea.

Madereva wa bajaji, malori, mabasi ya mikoani na daladala wafuate sheria na kanuni zilizowekwa, kupunguza na kutokomeza ajali ambazo hutokea kwenye kivuko au zebra, ambazo husababishwa na kutojali kunakofanywa na baadhi ya madereva wanaopuuza sheria.

# Mpango klabu kidijitali chachu kuendeleza teknolojia

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imesema ni muhimu kuanzishwa klabu za kidijitali kwenye taasisi za elimu nchini kama hatua muhimu katika kujenga kizazi chenye umahiri katika eneo hilo ambalo linaongoza dunia kwa sasa.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, akiongea katika mahojiano maalum kuhusu umuhimu wa klabu za kidijitali na namna zitakavyoiwezesha nchi kupiga hatua kiteknolojia, alisema lengo ni kuhakikisha kuwa klabu za kidijiti zinaanzishwa katika kila ngazi ya elimu Tanzania na kwamba TCRA kwa kushirikiana na wadau wengine wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wanatekeleza.

Dk. Bakari alisema TCRA imeanza kampeni hiyo nchi nzima kuelimisha wadau na kuhamasisha uanzishwaji wa klabu za kidijiti kwa hiari, kuanzia ngazi ya elimu ya chekechea, msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu.

"Mpango huu ni sehemu ya mkakati wa TCRA kuhamasisha ukuaji wa matumizi ya TEHAMA ambazo zinawezesha kutumia mifumo ya kidijiti na programu za TEHAMA katika ngazi zote za matumizi kwenye sekta mbalimbali," alisema.

Aidha, alisema uanzishwaji wa klabu za kidijiti ni msingi mkuu wa kuwezesha ubunifu wa ndani Tanzania na uvumbuzi unaolenga kutatua changamoto za maeneo husika kwa kutumia wataalamu nchini.

Kampeni inayoendelea inatekelezwa kupitia ofisi ya TCRA Zanzibar na ofisi za kanda. TCRA ina ofisi kwenye kanda tano – Mashariki (Dar es Salaam), Ziwa (Mwanza), Nyanda za Juu Kusini (Mbeya), Kati (Dodoma) na Kaskazini (Arusha).

Meneja wa Kanda ya Ziwa, Imelda Salum, alisema ni muhimu mchango wa klabu hizo kuwezesha vijana wa Kitanzania kupata stadi zinazohitajika kwa ajili ya kushiriki uchumi wa kidijitali.

Alisema klabu hizo zinaundwa kwenye ngazi zote za elimu na zitakuwa majukwaa muhimu ya kielimu yatakayozalisha wavumbuzi na viongozi wapya kwenye teknolojia.


"Vilabu vya kidijiti sio tu shughuli za ziada shuleni. Kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo wa TCRA wa uanzishaji wa klabu, hizi zitakuwa na majukwaa kwenye taasisi za elimu yatakayowapatia watoto na wanafunzi kuanzia chekechea hadi vyuo vikuu stadi za kidijiti wanazohitaji kufanikiwa kwenye uchumi wa kidijiti," alifafanua.

"Klabu hizi ni muhimu katika kujenga jamii inayoelewa, yenye stadi na uwezo wa kuchangia katika kufikia malengo yetu ya kitaifa, ambayo yatafanikiwa kwa kutekeleza kikamilifu mipango ya kujenga Tanzania ya kidijiti," alisema Imelda.

Alisema mpango huo pia unaenda sambamba na hatua za kuendelea masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM) na pia kuimarisha fikra za wanafunzi na uwezo wao wa kuvumbua na kwamba ziko wazi kwa wanafunzi wote wanaochukua masomo hayo.

Alisema uanzishaji, uendeshaji na uendelevu wa klabu hizi vinahitaji juhudi za ushirikiano wa wadau mbalimbali, pamoja na taasisi za elimu, wanafunzi, wazazi na walezi na jamii kwa ujumla.

Shule zitatoa na kuwezesha kutumika miundombinu, rasilimali na teknolojia, wakati wazazi na jamii wanategemewa kuunga mkono na kuhimiza vijana kuanzisha na kujiunga na klabu hizi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni na Mwakilishi wa Serikali ya Burundi, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani, Maendeleo ya Jamii na Usalama wa Raia, Theofile Ndarufatiye (kulia), wakibadilishana nyaraka za makubaliano ya utaratibu wa urejeaji wa wakimbizi wa Burundi wanaohifadhiwa nchini, mkoani Kigoma jana. Jumla ya wakimbizi 158,902 wanahifadhiwa nchini. **PICHA: WIZARA YA MAMBO YA NDANI**

# DRC, Tanzania watia saini mkataba kujenga bandari

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI za Tanzania na DRC zimetia saini mkataba wa kuimarisha Bandari ya Dar es Salaam kwa kuongeza manufaa ya kijiografia na ushindani kwenye shoroba kwa ujumla.

Mkataba huo ni kwa DRC kuipatia Tanzania eneo la hekta 60 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu nchini humo.

Mkataba huo ulitiwa saini na Naibu Waziri wa Uchukuzi Tanzania, David Kihenzile na Waziri anayeshughulikia masuala ya usafirishaji DRC, Marc Likombo na kushuhudiwa na makatibu wakuu wa wizara hizo huku nchi ikiwakilishwa na Prof. Godius Kahyarara na Balozi wa Tanzania DRC, Said Mshana.

Akizungumza baada ya kutiwa saini kwa makubaliano hayo, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Profesa Godius Kahyarara, alisema hatua hiyo ni muhimu kwa kuwa itawezesha Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) kutoa huduma ndani ya DRC na kuondoa ulazima wa wateja kuja mara kwa mara bandarini.

Alisema madereva wanaopeleka shehena DRC wataondokana na adha ya kusubiri kwa muda mrefu kwa kuwa mzigo ukifikishwa bandari kavu watakuwa na sehemu ya kukamilisha taratibu tofauti na hivi sasa ambapo kumekuwapo msongamano mingi barabarani wakisubiri ukamilishaji wa nyaraka. Aidha, alisema sekta binafsi nchini zikiwamo benki, wafanyabiashara wa bidhaa mbalimbali watakuwa na fursa ya kufungua biashara zao katika bandari kavu hizo ikiwamo masoko maalum.

Alisema bandari kavu hizo zitajengwa katika majimbo ya Katanga na Tanganyika.

Kwa mujiu wa Profesa Kahyarara, DRC inaagiza zaidi ya asilimia 80 ya vyakula pamoja na asilimia 90 ya bidhaa za viwanda ikiwamo vifaa vya ujenzi.

Aidha, alisema baada ya bandari kavu serikali kwa kushirikiana na ushoroba wa kati inaandaa mpango wa uwekezaji katika Ziwa Tanganyika kuwezesha Dar es Salaam kubaki kama lango kuu la nchi za ushoroba wa kati.

Akizungumza baada ya kutia saini mkataba huo, Naibu Waziri wa Uchukuzi Tanzania, David Kihenzile, alisema serikali imetenga jumla ya hekta 60 kati ya hizo 15 za ardhi zimetengwa katika eneo la Bandari Kavu ya Katosho - Kigoma na hekta 45 katika eneo la Kwala- Pwani sambamba na kutoa hati miliki kwa ajili ya nchi DRC kujenga na kuendesha bandari kavu.

Naibu Waziri Kihenzile alisema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha usafirishaji na uchukuzi unarahisishwa husani kwa mzigo mkubwa unaosafirishwa na DRC kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano wa DRC, Likombo alisema DRC imetenga hekta 15 katika eneo la Kasumbalesa na hekta 20 katika eneo la Kasenga-Jimbo la Haut Katanga; na hekta 25 katika eneo la Kasambondo-Kalemie Jimbo la Tanganyika sambamba na kutoa hati miliki kwa ajili ya Tanzania kujenga na kuendesha bandari kavu.

Pia serikali ya DRC imefanya hivyo ili kurahisisha biashara baina ya nchi hizo mbili kwani DRC inaitegemea sana Tanzania katika kusafirisha mizigo yake.

Mkataba huo unatarajiwa kuongeza ufanisi na idadi ya mzigo unaosafirishwa katika myororo mzima wa uchukuzi na kwamba takwimu zinaonyesha kwa 2022/23 tani milioni 3.5 za mzigo wa Kongo zilihudumiwa katika Bandari ya DRC.





KWA USALAMA WA TANZANIA IJAYO

Miaka 5 ya Benkibima (Bancassurance), Ujenzi wa Sekta Inayoshamiri na Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima Nchini

Sekta ya bima nchini inakua kwa kasi kubwa. Katika kuelezea mafanikio hayo Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), itachapisha matoleo maalum katika magazeti yake ya **The Guardian** na **Nipashe** mwezi ujao yatakayojikita kuangalia upatikanaji huduma za bima zenye matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Matoleo hayo yatajikita zaidi kuelezea:

- **Mafanikio ya Benkibima kwa Kipindi cha Miaka Mitano**
- **Jitihada za Kitaifa Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima**
- **Mwelekeo wa Sekta ya Bima katika Serikali ya Awamu ya Sita**

Mradi huu wa ujumuishi wa huduma za kifedha ni jukwaa linalotoa fursa ya kipekee kwa watoa huduma za bima na wadau wengine kuonesha jinsi wanavyochangia ongezeko la upatikanaji huduma za bima na mapokeo yake nchini.

Usikose kutumia nafasi hii adimu kunadi taasisi yako na suluhisho bunifu dhidi ya majanga.

**Ili kupata maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki:**
**Wasiliana nasi kwa simu: 0714 791747, 0763214317, 0753 01427**
**Barua Pepe: advertise@guardian.co.tz**

# Bank of India (Tanzania) Ltd.

*Relationships beyond banking*

## DISCLOSURES MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014 AND CONSUMER PROTECTION REGULATION, 2019
## MINIMUM DISCLOSURE OF CHARGES AND FEES (GHARAMA ZA HUDUMA ZETU)

### Service Charges (Exclusive of VAT and Government Levy on Digital Transactions)
### (The applicable VAT (Value added Tax) and Govt Levy on digital Transaction to be collected during the collection of service charges)

**A. REMITTANCE –OUTWARD**

| Sr. No. | Item | Charge in TZS or Equivalent to TZS |
|---|---|---|
| **TISS Remittance (**Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | Remittance -TZS or TZS Equivalent | |
| | Transaction value | |
| | Between TZS 1 to 10 million | 2,000 |
| | Between TZS 10 million to 50 million | 5,000 |
| | Above TZS 50 million | 10,000 |
| | | |
| **Other Outward Remittance** | 1USD up to 6,000 | USD 15 |
| | USD 6,001 – 10,000 | USD 30 |
| | Above USD10,000 | @ 0.35% Maximum USD 75 |
| Tracer Charges | Irrespective of Amount | USD 30 |
| Recall back funds charges | Irrespective of Amount | USD 30 |

**B. REMITTANCE –INWARD**

| Sr. No. | Item | Charge |
|---|---|---|
| (Only for A/c holders – Not permitted for non a/c holders) | From inside Tanzania | Free |
| | From outside Tanzania: as under | |
| | For Current /Overdraft Accounts | 0.35% of inwards remittance Minimum USD 18 Maximum USD 70. |
| | For Saving Accounts | |
| | USD 0 up to USD 100 | Free |
| | USD 101 up to USD 500 | USD 10 |
| | Above USD 500 | USD 18 |

**C. DEPOSIT AND RELATED SERVICES**

| Item | TZS A/c | USD A/c |
|---|---|---|
| **Saving Account :-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 2000 |
| Cash withdrawal charges over USD 2,000 to USD 5000 per day | — | 0.25% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | — | 0.60% of withdraw amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25 Mn per day | 0.10% of withdrawal amount | |
| Cash Deposit charges over USD 5,000 per day | — | 0.60% of deposited amount |
| Cash deposit charges for small currency USD notes ranging from USD 1 to USD 20, irrespective of amount deposited (i.e. both for below and above USD 5,000) | — | 12% (Min USD 1) of the aggregate small currency amount |
| **Current Account:-** | | |
| Cash withdrawal per day –Free of charge, up to amount | TZS 25 Mn | USD 5000 |
| Cash withdrawal charges over USD 5,000 per day | — | 0.60% of withdrawal amount |
| Cash withdrawal charges over TZS 25.00 Mn per day | 0.15% of withdrawal amount | — |
| Cash deposit charges over USD 10,000 per day | | 0.60% of deposit |
| **Maintenance of minimum balance: -** | | |
| For Saving Account-Without Cheque Book Facility | TZS 50,000 | **USD 50** |
| With Cheque Book Facility | TZS 200,000 | USD 200US D 200 |
| For Current Account | TZS 200,000 | **USD 200** |
| **Minimum balance charges (in case of non-maintenance of minimum balance)** | | |
| Saving Account - Without cheque book | TZS 900 p.m | USD 4 p.m |
| With cheque book | TZS 3600 pm | USD 15 p.m |
| Current Account- | TZS 20,000 p.m | USD 15 p.m |

**D. Other Common Charges**

| Item | Charges: TZS A/c | Charges: USD A/c |
|---|---|---|
| Stop Payment Instructions | TZS 35,000 | USD 28 |
| Regular statement of a/c (Monthly) | Free | Free |
| Interim/additional statement | TZS 1500 per page | USD 1.50 per page |
| Issue of bankers' cheque | TZS 40,000 | USD 30 |
| Cancellation of bankers cheque/DD | TZS 20,000 | USD 15 |
| Issue of Duplicate Bankers cheque/Demand Draft/ Duplicate FDR | TZS 30,000 | USD 20 |
| Application charge for Treasury Bond | TZS 100,000 | USD Equivalent to TZS 100,000 |
| Issue of Balance certificate (Saving Account) | TZS 20,000 | USD Equivalent to TZS 20,000 |
| Issue of Balance certificate (Current Account) | TZS 50,000 | USD Equivalent to TZS 50,000 |
| Signature verification and Photo Attestation charges for Domestic A/c Holders | TZS 10,000 | USD Equivalent to TZS 10,000 |
| Verification of Documents such as KYC Documents along with verification of Photo and Signature of Customer Mentioned account with Bank of India- in India /Overseas | TZS 25,000 | USD Equivalent to TZS 25,000 |
| Savings bank customer Identification card- One time | TZS 20,000 | USD 10 |
| Dormant a/c Activation Per Activation Fees | Individual TZS 5,000<br>Corporate TZS 12,000 | Individual USD 3<br>Corporate USD 6 |
| Account Freezing/un freezing Charges | Free | Free |
| SMS Alert facility | Free | Free |
| Email Alert Facility | Free | Free |
| Monthly Statement on Registered Email | Free | Free |
| Balance Inquiry (Over the Counter) | Free | Free |
| Charges for Deletion of Decease Person Name from the Saving Account | Free | Free |
| Charges for Addition/modification Account such as Change in respect of Corporate A/c | TZS 20,000 | USD 10 |
| Updating of Mobile No. in A/c (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Change /Modification in Address (SB,CD,OD) | Free | Free |
| Issuance of No Dues Certificate for Non-Borrowers. | TZS 10,000 | USD 7 |
| Ledger Folio Charges per Folio (40 lines per Folio) only for Current and Overdraft Accounts | TZS 6,000 per Folio | USD 4 per Folio |
| Postages/Courier Charges<br>Inland/Foreign | TZS 30,000 or actual charges whichever is higher | USD Equivalent to TZS 30,000 |

**E. CLEARING SERVICES**

| Item | Charge/Fees: TZS A/c | Charge/Fees: USD A/c |
|---|---|---|
| Within walking distance-1 km | TZS 70,000 | USD 45 |
| Far off distance –more than 1 km | TZS 95,000 | USD 65 |
| Cheque returned charges –financial reasons (inward/outward) | TZS 70,000 | USD 55 |
| Inward/outward cheque collection -USD | 0.60% Min comm.18 postages 90 | 0.60% Min comm.18 postages 90 |

## CREDIT MATTERS

| Item | Charge/Fees |
|---|---|
| **Proposal Processing Charges: -** | |
| New Overdraft/Term Loan/Demand Loan | 1.50% of sanctioned limit<br>(Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| TOD/TOL/ADHOC | Proportionate to 1.50% for TOL/TOD/ADHOC Period minimum USD 60 |
| New NFB BG/LC Facility | 1.50% of sanctioned limit (Regular Limit – 1.50% for 12 Months) |
| Review of Overdraft Limit | 1.50% on entire sanctioned amount. |
| Review of Term Loan Demand Loan Personal Loan Vehicle Loan Loan Against Property Etc. | 0.15% maximum USD 600 or TZS 1.20Mn on the reviewed amount and 1.50% on the additional Term Loan /Demand Loan amount. |
| Schematic Lending up to 36 months/Staff Loan | Nil |
| Prepayment charges | 2.50% of the prepaid loan amount. |
| Documentation charges for New Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan/Non Fund base Limit | Actuals as per advocate Bill + 0.30% handling charges<br>1) No Documents charges would be applicable for TOD/TOL/ADHOC Limit, however actual expenses if any to be recovered.<br>2) Documentation charges also NOT Recoverable for the Loan/Overdraft against FDR. |
| Charges for Amendments/Modification of Sanction Terms | 0.25% on the sanctioned limit<br>**We enumerate the illustrative instances of Modification in Terms and Conditions to be effected at the request of the Borrower where this charge will be levied: -**<br>1) Substitution of Collateral Securities/Personal Guarantee<br>2) Release of Personal Guarantee/Collateral Security.<br>3) Interchangeability of limits.<br>4) Change in project/items of Machinery<br>5) Ceding of charges on assets(Pari-Passu)<br>6) Restructuring, Replacements of Loans/ Deferment of Loan installments.<br>7) Approvals for mergers & amalgamations.<br>8) Any other miscellaneous credit related approvals. |
| Revalidation of Sanction | **25% of Applicable PPC Charges on Overdraft Limit/Term Loan/Demand Loan** |
| Lead bank Charges | **USD 1000 or equivalent in TZS per annum/one time** |
| Fee for Opening Escrow/TRA A/cs (Trust and Retention A/cs) | **Where**<br>**We are Lead bank: Nil**<br>**We are Not Lead Bank:**<br>USD 500 or equivalent in TZS per annum/one time |
| Charges for Supplying copies of Loaning Documents to Customer. | First instance: Free<br>**USD 10 or equivalent in TZS for further requirement.** |
| Non/Delayed Submission of Audited Financial Statements of the Company OR wherever applicable | **USD 100 or equivalent in TZS per month or part thereof**<br>**Note:-**Audited Financial statements of the firm/company within 6 months from closure of Financial Year or as approved by TRA for the relevant year. |
| Inspection charge | **TZS 50,000** or equivalent to USD per visit /inspection or at least once in quarter whichever is higher.<br>**Note:-**<br>1) Out of Pocket Expenses to be recovered additionally along with regular inspection charges wherever applicable<br>**2) Project Monitoring Inspection Charges/Technical Due Diligence Inspection charges:** Considering the fact that this inspection is proposed for safeguarding banks Interest, normal inspection charges besides travelling, boarding/lodging expenses are to be recovered from the borrower. |
| Issuance of No objection certificate (NOC) | **USD 100 or equivalent in TZS** |
| 1st party/3rd party Overdraft/Loan against deposit of our Bank (BOITL) | Waiver of Processing & Documentation charge. |
| Overdraft/Term Loan/Demand Loan Conversion Charges (Currency Conversion) | For Overdraft account 0.50% of Sanction Limit.<br>For Term Loan/Demand Loan 0.50% of O/s Amount |
| Earmarking of Limits | **USD 500 or equivalent in TZS per annum** |
| Non Compliance of Sanction terms/Commitment charges | **1.00% additional Penal Interest to be charge till compliance of Sanction terms** |

**D&B/ Other Credit Information Search for per Borrowal a/c (New/Additional/Review of limit)**

| | USD Facility | TZS Facility |
|---|---|---|
| Up to TZS 20 Mn/USD 10,000 (Only for new and additional Limit. **Review – No charge**) | USD 5 | TZS 5,000 |
| Over USD 10,000 to USD 50,000/ Over TZS 20 Mn up to TZS 100 Mn | USD 10 | TZS 20,000 |
| Over USD 50,000/TZS 100 Mn | USD 50 | TZS 100,000 |
| D&B Search for non-Borrower, on request | USD 50 | TZS 100,000 |
| Charges for Furnishing copy of Credit Information report obtained from CIC | **TZS 20,000** | **USD 10** |

| Item | Charge |
|---|---|
| **Guarantee (Performance/Financial) :-** | |
| Guarantee Commission | 1.35% per quarter or part thereof minimum for one quarter. |
| Guarantee against 100% cash margin | 50% concession on the above rate |
| Swift Charges | **As Applicable** |
| Postages | **As Applicable** |
| Revert of Guarantee before Expiry | **Minimum 1 Qtr BG Commission to be recovered for part of quantum of full guarantee commission to be recovered** |
| Closure of Guarantee After Expiry of Claim Period | Nil |
| Invoke of Guarantee | **USD 200 or equivalent in TZS** |
| | **A. Financial Guarantees: -**<br>1. In favour of Customs/Excise/Tax Authorities towards tax/Duties payment Etc.<br>2. Favouring Courts for Release of Amounts.<br>3. For Guaranteeing Loan payments.<br>**B. Performance Guarantees: -**<br>1. In lieu of earnest money deposit<br>2. In lieu of tender deposit<br>3. In lieu of security deposit<br>4. To obtain advance payments (generally exports)<br>5. To obtain mobilization advance (generally domestic)<br>6. Towards Direct/indirect taxes to govt. in respect of specific transaction.<br>7. For Direct/indirect taxes disputes with tax Authorities.<br>8. For payment for supplies/services made /rendered<br>9. For Securing retention amount<br>10. For Bidding/tendering for Project Contacts<br>11. For Performance in terms of any agreed contact.<br>**Note: - No processing charges or documentation charges are to be levied in case of Casual BG limits issued against 100% or more cash margin.** |
| **Imports :-** | |
| LC Opening charges | 1.35% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| Against 100% cash margin | 50% concession on the above rate i.e. 0.67% per quarter +SWIFT charges USD 75/- |
| LC Amendment Charges | Per amendment 0.40% of LC amount (minimum USD 60 and Maximum USD 325) +SWIFT charges USD 30 (Same for LC against 100% cash margin) |
| Acceptance of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 180 |
| Retirement of bills under LC | 0.60% of Bill amount Min USD 30 Maximum USD 360 |
| Inward Bills for Collection | 0.30% of Bill amount minimum USD 150 |
| **Exports:-** | |
| Negotiation of Bills under LC | 0.60% of Bill amount Minimum USD30 Maximum USD 360 |
| Confirmation of Export LC | 0.90% per quarter +SWIFT charges USD 30/- |
| LC Advising Charges | USD 150 |
| Export Bills for Collection | 0.60% of Bill amount Minimum USD 30 Max USD 360. |
| Charges for Certifying invoices subsequent to negotiation | **USD 10 Per Invoice** |
| Clean payment Received under LC | **USD 100 per occasion** |
| Advice of transfer in transferable LC | **USD 100 per advice of transfer and acceptance commission at 0.30% Minimum USD 100** |

### OTHER DISCLOSURES
### (VIAMBATANISHI NYINGINEZO)

| No. | ITEM/TRANSACTION | USD | TSHS |
|---|---|---|---|
| **1.0** | **Base or Prime Lending rate** | 7.50% p.a. | 14.50% p.a. |
| **2.0** | **Maximum Spread above Base or Prime Lending rate** | 7.00% | 7.00% |
| **3.0** | **Penal interest** | | |
| a) | For Non Compliance of Terms of sanction | 3% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| b) | For Overdrawing/ Excess Drawings due to non – payment of interest/ Instalments/ Charges | 5% p.a. over Regular Rate of Interest | |
| **4.0** | **Deposit Rate** | | |
| i) | Current Deposit | Nil | Nil |
| ii) | Savings Bank Deposit | 0.50% p.a. | 2.50% p.a. |
| iii) | Fixed/Recurring/QIC/MIC deposit | **Up to USD 10,000** | **Up to TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.00% | 6.25% |
| | Over 6 months | 3.50% | 7.25% |
| | | **Over USD 10,000** | **Over TZS 10,000,000** |
| | 6 months | 3.50% | 6.75% |
| | Over 6 months | 4.00% | 7.75% |
| | * No interest is payable in case of premature withdrawal of fixed deposits | | |

**No Penalties & Other sanctions have been imposed by Bank of Tanzania (BOT)during the Period covered by the Disclosure**

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name. | Designation | Signature | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Antaryami Sarangi | Managing Director | Signed | 08.06.2024 |
| 2. | Heriabdiel Ayoh | General Manager | Signed | 08.06.2024 |
| 3. | Robert Kibona | General Manager | Signed | 08.06.2024 |



## Watakiwa kutambua karama ya mtoto wa kike

**Na Getrude Mpezya,** ARUSHA

MISS Tanzania wa zamani, Faraja Nyalandu, amewapa somo viongozi wa koo na mila wa jamii ya kifugaji wa kimasai wa Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha, akiwataka kutambua karama ya mtoto wa kike wa jamii hiyo anavyoweza kubeba ndoto au maono ya familia zao kiuchumi.

Amesema katika Wilaya ya Monduli, wakazi wake hasa jamii ya kimasai wanapaswa kuachana na mila potofu na kandamizi za kuacha kuficha watoto wenye ulemavu ndani na kuwapeleka shule, wakiwamo watoto wa kike.

Alizungumza hayo jana jijini Arusha, wakati wa uzinduzi wa mradi wa 'Nijali' ulioanzishwa na Shirika lisilo la kiserikali la Okoa New Generation (ONG).

"Badilisheni maisha ya mtoto wa kike, kwa kufanikisha ndoto zake na kuacha kuwaficha ndani watoto hao na badala yake watoeni nje ili kukuza zaidi mazingira ya elimu kwa watoto wenye ulemavu.

"Wanapaswa kuwatengenezea mazingira rafiki yatakayowasaidia wao kubadilisha maisha ya mtoto wa kike. Kwa kushirikiana na serikali kupitia maofisa elimu kata na wakuu wa shule, tumeweza kujadili mustakabali wa elimu katika Wilaya ya Monduli, kwa kumgusia kwa kipekee mtoto wa kike, hasa yule mwenye ulemavu, kwa kuangalia vikwazo na changamoto zinazopelekea mtoto wa kike kukosa elimu bora.

Zaidi aliongeza: "Nafurahi kuona kwamba mradi huu unaenda kugusa moja kwa moja maisha ya watoto wa kike katika jamii za kimasai na kushirikiana kwa karibu sana na wanajamii wote."

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Okoa New Generation, Neema Mgendi, alisema lengo la kuanzisha mradi huo ni kuhakikisha mtoto wa kike aliyeko pembezoni mwa mji, mwenye ulemavu hasa katika miji yenye mifumo dume, anapopata haki zake.

"Katika Wilaya ya Monduli, zipo shule zinazopokea watoto wenye ulemavu, lakini katika shule hizo, hakuna mtoto mwenye ulemavu wa jamii ya kimasai aliyepelekwa shule; wengi waliopo wanatoka mikoa mbalimbali," alisema.

Kwa mujibu wa Mgendi, hali hiyo inawapa picha kwamba bado jamii za pembezoni, hasa kwa wale ambao wana mfumo dume, mtoto wa kike mwenye ulemavu kupelekwa sekondari si kitu rafiki.

Neema Mgesa, binti mwenye ulemavu, anayesoma kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Manyara, aliiomba serikali kutengeneza miundombinu bora kwa walemavu shuleni, hasa njia wanazotumia kuingia darasani pamoja na matundu ya vyoo.

# Makada 44 CHADEMA wajitosa katika uchaguzi Moshi Mjini

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MCHAKATO wa uchaguzi wa viongozi ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Kanda ya Kaskazini umeshika kasi baada ya makada 44 kujitosa kugombea uongozi wa Jimbo la Moshi Mjini, mkoani Kilimanjaro.

Jimbo la Moshi Mjini, lilikuwa likiongozwa na mgombea ubunge wa CHADEMA mwaka 2020, Raymond Mboya, Meya wa zamani wa manispaa hiyo.

Jana, Katibu wa Kanda ya Kaskazini wa CHADEMA, Amani Golugwa, aliiambia Nipashe kwamba uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025, patakuwa hapatoshi kwenye majimbo 35 ya mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Manyara.

"Kwa Kanda ya Kaskazini, ndiyo tuko kwenye mchakato wa uchaguzi. Bado tuko katika ngazi ya majimbo na wiki hii tutakuwa na chaguzi kadhaa kwenye kanda yetu.

"Sasa hivi tunawafanyia interview (usaili) wagombea wote wa chama na mabaraza, tunawafanyia usaili. Tuko kwenye hatua ya uchaguzi ndani ya majimbo na ninavyozungumza jana (Jumapili), tumekamilisha usaili kwenye uchaguzi ambao tumeutangaza tayari, ni wa Moshi Mjini (Manispaa).

...Ndio Jimbo la kwanza tumeanza na tulikuwa na jumla ya wagombea 44 na wagombea 43 wameteuliwa. Mmoja hakukidhi vigezo. Hawa ni wagombea wa nafasi mbalimbali ngazi ya jimbo."

Wakati mtifuano huo ukiendelea majimboni, inaelezwa kuwa vigogo wanne wa kanda hiyo nao wananyemelea nafasi ya Mwenyekiti wa Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema anayemaliza muda wake.

Mei 30 mwaka huu, Lema ambaye ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA aliandika kupitia akaunti yake ya mtandao wa X, kuwa hatagombea tena nafasi hiyo.

Baada ya kauli yake makada wanne walioonyesha nia ya kumrithi wamo Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake (BAWACHA)- Kilimanjaro na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, Grace Kiwelu na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Yosepher Komba.

Wengine ni Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Kilimanjaro, Michael Kilawila na Gervas Mgonja, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Kanda ya Kaskazini.



Katibu wa CCM Taifa, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, akiwahutubia wananchi wa Mkoa wa Tanga katika Viwanja vya Namore juzi, pia alizungumza na wananchi wa mji wa Korogwe pamoja na kuzindua kiwanda cha kutengeneza nyaya za umeme cha Tanga Cable kilichoko jijini humo wakati wa ziara yake mkoani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Maabara ya kuhifadhi wadudu yaanzishwa

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

SERIKALI imeanzisha maabara maalumu ya kuwahifadhi wadudu wanaopatikana nchini na nchi nyingine duniani, ili kuandaa orodha ya makundi mbalimbali ya wadudu na mtawanyiko wao.

Wadudu hao ni pamoja na nyuki, mbawakawa wanaoviringisha vinyesi, wadudu wa maji baridi na mbawakawa wanaoishi ardhini.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Angelah Kairuki akizungumza jana Jijini Arusha, alisema serikali inatamani kuona wadudu sasa nao wanakuwa sehemu ya utalii wa kimataifa.

"Taasisi yetu ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), naipongeza kwa kuthamini umuhimu wa wadudu katika sekta ya uhifadhi na kuanzisha maabara maalumu ya kuwahifadhi wadudu wote wanaopatikana hapa nchini na nchi nyingine.

"Maelekezo yangu kwenu nataka kuona taasisi hii ikiziona fursa za utalii katika suala zima la wadudu," alisema.

Mtafiti wa Wadudu wa TAWIRI, Neema Kilimba, akitoa taarifa kuhusu maabara hiyo, alisema taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine inakamilisha kanzidata ya makundi mbalimbali ya wadudu wanaopatikana Tanzania na nchi nyingine.

Aidha, alisema TAWIRI inajivunia kuwa na maabara hiyo ya wadudu ambayo ni kituo muhimu na sahihi kwa ajili ya kuhifadhi makundi mbalimbali ya wadudu yanayofanyiwa utafiti.

Kupitia maabara hiyo, TAWIRI inaandaa orodha ya makundi mbalimbali ya wadudu na mtawanyiko wao nchini wakiwamo nyuki, mbawakawa wanaoviringisha vinyesi, wadudu wa maji baridi na mbawakawa wanaoishi ardhini.

Kwa mujibu wa Kilimba uwapo wa kanzidata hiyo ya makundi mbalimbali ya wadudu, itasaidia kutambua aina za wadudu zilizoko nchini, makazi na mtawanyiko wao, hivyo kuchochea uhifadhi wa bioanuwai hiyo muhimu, kutoa elimu na msingi wa takwimu kwa watafiti na wanafunzi.

Wadudu wanachangia uchavushaji wa mimea kwa zaidi ya asilimia 80, uozeshaji na umeng'enyaji wa taka, hususani vinyesi na usafishaji wa mazingira, uoteshaji wa mbegu mbalimbali, uongezaji mbolea kwenye udongo na kuwezesha makazi ya wanyama wengine.

Pia wadudu ni chakula kwa wanyama wengine na sehemu muhimu kwenye mzunguko wa chakula.

Taarifa ya mtafiti huyo pamoja na mambo mengine inaeleza kuwa wadudu wanatumika kama viashiria vya afya ya mifumo ya kiikolojia na wanachangia kwa asilimia kubwa, kuongeza kipato kwa jamii kwa kuuza wadudu wenyewe kama chakula au bidhaa zitokanazo na wadudu.





# Wanafunzi 'vinara' kutaka dawa mvuto wa mapenzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA wa jadi katika Kata ya Kagongwa, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga wamesema wamekuwa wakipokea idadi kubwa ya wanafunzi wanaotaka dawa za mvuto wa mapenzi maarufu kama samba, ili wapate wanaume wenye fedha.

Wamesema kinachowachochea wanafunzi hao kutafuta dawa hiyo ni kutokana na baadhi ya wazazi na walezi wao kuendekeza mila hizo kwa kutaka kupata mali mapema, hali inayosababisha wanafunzi wengi kukatisha masomo na kujiingiza katika vitendo vya ngono wakiwa na umri mdogo na kupata mimba pamoja na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Walieleza hayo juzi wakati wa kikao kilichowakutanisha viongozi wa madhehebu ya dini, waganga wa jadi, wazee, waendesha bodaboda na vijana.

Lengo la kikao hicho ni kupunguza matukio ya ukatili wa kijinsia kwa wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

Akizungumzia adha hiyo katika kikao hicho, mmoja wa waganga wa jadi, Jongela Heneriko, alisema wanafunzi wanaongoza kuwatembelea kwa kutaka kuogeshwa dawa za mvuto wa mapenzi, kwa lengo la kutaka wanaume wenye uwezo wa kifedha ili kukidhi mahitaji yao ya shule.

Alisema kitendo cha wanafunzi kuja kuomba dawa hizo kinasababishwa na wazazi wenye tamaa ya kupata mali, hususani kipindi cha mavuno ambapo ndoa nyingi hufungwa.

Alisema kumekuwa na utamaduni usiokuwa na tija wa kutafuta dawa za mvuto, ili kuwavutia wanaume ambao wameuza mazao na kupata fedha.

"Kipindi hiki ni cha mavuno ya mazao mbalimbali na vijana, wanaume na wazee wanakuwa na fedha baada ya kuuza mazao, hatua inayofanywa ni kutafuta mabinti wadogo na kuanza nao mahusiano ya kimapenzi bila kujali ni wanafunzi na wana umri chini ya miaka 18, hili imekuwa ikitokea kipindi pia cha likizo za wanafunzi," alisema Heneriko.

Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Kituo cha Polisi Kagongwa, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi, Joseph Kyakalaba, alisema amekuwa wakipokea kesi nyingi za watoto kufanyiwa ukatili wa kingono na watu wazima kwa kuwalaghai kwa pombe na fedha.

Alisema hayo yamekuwa yakisababishwa na wanaume baada ya kuuza mazao na kukimbilia mjini kufanya sterehe na wanawake wanaofanya biashara ya ngono, huku wakiacha familia zikiangaika kwa kukosa chakula ndani.

Hivyo, aliwaomba viongozi wa madhehebu ya dini kukemea masuala haya kila wanapofanya ibada zao.

Aidha, Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Kahama, Swaiba Chemchem, aliwataka makundi hayo kuacha mila potofu ambazo ni kandamizi na badala yake wawape fursa watoto wa kike kusoma ili watimize ndoto zao.

Mchungaji wa Kanisa la EAGT Ebenezer Kagongwa, Paul Kingu alisema kwa kila vikao ambavyo watakuwa wakivifanya na waumini wao watahakikisha kunakuwa na ajenda ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa kueleza madhara yake.

Aidha, aliwasisitiza waganga wa jadi kuachana na mila hizo na kufanyakazi kwa kuzingatia miiko yao.




Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi, akionyesha barua walionyimwa uwanja wa kufanya mkutano wa hadhara na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Madiwani wataka unafuu bei za pembejeo

**Na Mwandishi Wetu,** SENGEREMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema wameiomba serikali kusimamia uuzwaji wa pembejeo ikiwamo mbegu za mazao.

Wamesema lengo la kufanya hivyo ni kuhakikisha wananchi wanapata mbegu hizo na kulima kisasa ili kupata mavuno mengi tofauti na sasa.

Madiwani hao akiwamo Diwani wa Kata ya Bungolo, Musa Ngazila, wakati wa maswali katika kikao hicho aliomba kama kuna uwezekano mbegu hizo ziwekewe ruzuku kama ilivyo kwa mbolea, kwamba gharama zake zipo juu zaidi ya mavuno yanayopatikana.

Alisema hatua hiyo itawasaidia wakulima wa chini kutumia mbegu za kisasa kuliko wanavyolima na mbegu za kawaida hali inayosababisha kupata mavuno kidogo na kushusha mapato ya mkulima na halmashauri.

Diwani wa Kata ya Bupandwa, Masumbuko Bupamba, alisema uchumi wa Buchosa unategemea kilimo, hivyo suala la gharama za mbegu kuwa juu na mazao kuuzwa kwa bei ndogo linarudisha nyuma juhudi za wakulima pamoja na shughuli hizo za kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Benson Mihayo, alisema serikali imekuwa ikifanyia kazi suala hilo ikiwa ni pamoja na kuweka ruzuku kwenye mbolea na kuhusu gharama za mbegu atalifikisha sehemu husika ili kilimo kwa wananchi wa Buchosa kiendelee kukua.

## Elimu yawaokoa watoto wenye ulemavu Iselamagzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI katika Kata ya Iselamagzi wilayani Shinyanga waliokuwa wanawaficha ndani watoto wenye ulemavu wameacha tabia hiyo baada ya kupewa elimu.

Hayo yalibainishwa hivi karibuni na Ofisa Mtendaji wa Kata hiyo, Amos Daudi, wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema awali wazazi kwenye kata hiyo walikuwa na tabia ya kuwaficha ndani watoto wenye ulemavu na hata kuwanyima haki zao mbalimbali ikiwamo ya kupata elimu.

"Zamani watoto wenye ulemavu hapa Iselamagzi walikuwa wanafichwa ndani, sasa hivi tabia hiyo haipo tena na wengi walipelekwa shule na wanasoma Shule ya Msingi Iselamagazi," alisema Daudi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Iselamagazi, Elias Litubija, alisema shule hiyo ni ya mchanganyiko, inachukua pia watoto wenye ulemavu.

Hivyo, alitoa wito kwa wazazi kuendelea kuwapeleka shule watoto wao wenye mahitaji maalumu ili wapate elimu na kutimiza ndoto zao.

Baadhi ya wazazi wa kata hiyo ambao wana watoto wenye ulemavu walilieleza Nipashe kuwa watoto hao walikuwa wamewachukulia kama mkosi kwao na ndiyo maana walikuwa wakiwaficha ndani.

Walisema baada ya kupewa elimu na kupata ufahamu wamechukulia kama watoto wengine na kuamua kuwapatia haki yao ya elimu.

**"Zamani watoto wenye ulemavu hapa Iselamagazi walikuwa wanafichwa ndani, sasa hivi tabia hiyo haipo tena na wengi walipelekwa shule na wanasoma Shule ya Msingi Iselamagazi," alisema Daudi.**



Ukurasa 12

**Mabadiliko ya tabianchi yanakoroga rangi baharini**



Ukurasa 13

Kuboresha utaalamu kiafya kunavyoifanya Tanzania shamba darasa la sekta ya tiba



Ukurasa 14

**Kutamka, kuandika 'apana, akuna, amna' kunavyokichafua Kiswahili**


Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Jumanne Juni 11, 2024


ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Ni zama za magari yanayojiendesha

## • Yana ufanisi hakuna ajali, husoma, huelewa mazingira

DUNIA ya sayansi na teknolojia, inatamani kila kitu kifanywe na mashine au roboti na mwanadamu, awe pengine anapumzika muda wote.

Na sasa teknolojia imeingia kwenye kutengeneza na kuyafanyia majaribio magari yanayojiendesha yenyewe, yasiyohitaji yeyote kukalia usukani.

Yakipewa majina kadhaa, kuanzia gari linalojiendesha 'autonomous cars' au AC, gari lisilo na dereva, robotaksi au gari roboti kwa ujumla hufanya kazi bila kuendeshwa na binadamu.

Teknolojia ya magari yanayojiendesha yenyewe tayari imeshayaweka barabarani yakiwa na uwezo wa kusafiri na kujiendesha kwa maelfu ya kilomita, kupanda milima na kuvuka mabonde, bila kuhitaji dereva anayeshika usukani au kusaidia chochote.

Magari haya hutumia vitambuzi na teknolojia mbalimbali, kama vile rada, miongozo ya kielektroniki na yana uwezo wa kuona, kutafsiri na kutambua mazingira yanayopita au kukatisha kuanzia barabarani mijini, mbugani na mitaani huku yakifanya maamuzi ya kuendesha gari bila msaada wa binadamu.

Baadhi ya magari hayo yanajiendesha kikamilifu, kumaanisha kwamba yanaweza kushughulikia vipengele vyote bila kuongozwa.

Lengo la teknolojia ya magari yanayojiendesha ni kuboresha usalama, ufanisi na urahisi katika usafiri lakini pia kupunguza vifo vinavyotokana na makosa ya binadamu. Magari roboti hutumia teknolojia mbalimbali ili kujisogeza na kujiendesha yenyewe ambazo ni pamoja na 'sensorer', rada, lidar (kifaa kinachotumia mwanga na kufanya utambuzi), mifumo ya kamera ili kutambua mazingira yao na kuelewa mkao na mwendo wa vitu vingine vilivyo pembeni.



Gari roboti likiwa barabarani. **PICHA: MTANDAO**

Kuna GPS, hiki ni kifupisho cha Global Positioning System -GPS, ni teknolojia ya kuwezesha gari kujiweka kwenye ramani na kuonekana, huku likielekea sehemu au mahali linapokwenda.

Computer Vision, ni teknolojia nyingine ambayo gari husoma kile inachokiona kwenye kompyuta iliyo karibu na usukani, kisha kuchanganua na kutafsiri picha na video kutoka kwenye mifumo ya kamera iliyoko na kuelewa kinachoendelea katika mazingira yanayolizunguka gari barabarani.

'Machine learning', gari roboti hujifunza kwa kutumia mashine, ambayo ni kanuni za kujifunza kwa huruhusu kuboresha ujuzi wake, kutambua hali ilivyo kwa kuendesha baada ya muda, kuchanganua data kutoka kwa vitambuzi mbalimbali na kufanya maamuzi kulingana na taarifa inazozipata.

Mifumo ya udhibiti, kwenye gari roboti inahusika na kutafsiri data kutoka kwenye vitambuzi na kufanya maamuzi ya kuendesha gari kulingana na taarifa hizo. Mifumo hii ni pamoja na uendeshaji wa gari, kuongeza kasi na breki.

Mifumo ya mawasiliano: Katika gari hili kazi inaratibiwa na mifumo madhubuti ya mawasiliano ambayo huruhusu magari yanayojiendesha yenyewe kuwasiliana na magari mengine ya namna hiyo barabarani, kutambua miundombinu mingine kama vile taa za trafiki, vivuko vya wanaotembea, kona kali na alama zote za usalama ili kuratibu mienendo yake na kuboresha usalama zaidi.

### FAIDA ZINAZOTAZAMWA

Usalama, unatajwa kuwa ndilo jambo kuu. Magari yanayojiendesha yana uwezo wa kupunguza kwa kiasi kikubwa idadi ya ajali za barabarani na vifo vinavyosababishwa na makosa ya kibinadamu.

Ufanisi, ni sifa ya magari haya yanayoweza kuboresha mtiririko wa magari babarani na kupunguza msongamano, pia kuna matumizi ya nishati safi na kwa kuboresha uendeshaji.

Kuyafikia kwa uhakika bila usumbufu na udanganyifu, yanaweza kutoa chaguo la usafiri kwa wateja ambao hawawezi kuendesha gari kwa sababu ya umri, ulemavu na dharura.

Urahisi, ni jambo jingine muhimu kwa magari yanayojiendesha yanaweza kuruhusu watu hasa madereva kutumia muda wao kwa manufaa zaidi kama vile kufanya kazi badala ya kuendesha gari ziku zote, wengine kupumzika, badala ya kuendesha gari usiku na mchana.

Mlinzi wa mazingira, magari haya yanaweza kupunguza utoaji wa hewa chafu kwa kuboresha mifumo inayotumia nishati mseto kama umeme na gesi badala ya dizeli na petroli zinazochafua mazingira.

### YANAPOTUMIKA

Nchini China mambo yameanza kubadilika magari yasiyo na dereva hutumiwa katika majiji ya Beijing, Chongqing , Wuhan, Hubei na Shenzhen.

Kwa upande wa Marekani kufikia mwaka huu 2024, hakuna gari kamili kwa kiwango cha ukamilifu linaloweza kujiendesha lenyewe.

Lakini kuanzia Desemba 2020, kampuni ya usafiri ya Waymo ilikuwa ya kwanza kutoa usafiri wa teksi zinazojiendesha zenyewe kuhudumia umma, lakini si kwa ukamilifu, zilihitaji msaada wa binadamu.

Zilikuwa zinafanyakazi maeneo machache na kufikia Aprili 2024 Waymo inatoa huduma kwa majiji ya Arizona (Phoenix) na California (San Francisco na Los Angeles).

Barani Asia, India kampuni za TATA, Mahindra na Taasisi ya Teknolojia ya India (IIT) Madras ni kati ya mashirika yanayofanya kazi kwenye teknolojia ya magari yanayojiendesha na kuna matumaini kuwa huenda kukawa na mafanikio.

Taarifa hii ni kwa mujibu wa mitandao ya Analyticssteps na Taasisi ya Teknolojia ya India ya ITT Madras.

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Mabadiliko ya tabianchi yanakoroga rangi baharini

• Inaanza kuwa kijani bluu ikitoweka



Bahari inapohofiwa kujaa 'magugu maji'. **PICHA: MTANDAO**

UTAFITI wa hivi karibuni unaeleza kuwa bahari zinabadilika kuwa kijani kibichi na hilo huenda linachangiwa na mabadiliko ya tabianchi. Pengine ni matokeo ya kupenya joto kali na mwanga zaidi.

Mara nyingi rangi ya bahari ni ya bluu iliyokolea. Ndani ya bahari kuna 'phytoplankton' ndiyo inayoonyesha rangi ya kijani.

Ndio msingi wa mtandao wa chakula cha viumbe wa baharini ambao hudumisha maisha ya viumbe wadogo kwa wakubwa zaidi hatua kwa hatua kuanzia samaki na ndege wa baharini pamoja na mamalia (wanaonyonyesha).

Phytoplankton pia ni misuli katika uwezo wa bahari wa kukamata na kuhifadhi kabonidioksidi. Kwa hivyo wanasayansi wana nia ya kufuatilia phytoplankton katika uso wa bahari na kuona jinsi inavyoweza kukabiliana na mabadiliko ya hali ya hewa.

Kwa lugha nyingine phytoplankton ni viumbe vya baharini, wanaoofanana na utando wa kijani ndivyo vinavyotengeneza tabaka la chakula cha baharini.

> Lakini kuongezeka kwa joto la bahari, na kusababisha athari zaidi katika chakula na samaki wanaotegemea viumbe hawa ni jambo linalohofiwa.

Ingawa baadhi ya maji yanazidi kuwa ya kijani kibichi, hasa karibu na Ikweta, mengine yanakuwa bluu zaidi huku halijoto duniani ikiongezeka.

Ingawa mabadiliko haya ya rangi hayaonekani kwa macho, tafiti za setilaiti zinaonyesha kuna jambo la kubadilika rangi baharini.

Maji yenye rangi ya bluu iliyokolea yanaakisi kuwepo na maisha kidogo na hiyo ndiyo asili ya bahari, ilhali maji ya kijani kibichi yanaonyesha kuwapo kwa mifumo ikolojia, na hasa phytoplankton ambayo ni mimea inayopatikana kwa wingi kwenye bahari ya juu na ambavyo vina klorofili ya rangi ya kijani kwa kuchukua mwanga wa juu kutengeneza chakula.

Lakini kuwapo na kijani kingi ndani ya bahari kunawezekana kuwa na magugu bahari, au jambo geni linalotokea ndani ya maji hayo yanye chumvi nyingi, ukihitajika zaidi utaalamu na utafiti.

Ripoti ya hivi karibuni ya Hali ya Hewa huko Ulaya, iliyochapishwa Aprili 2024 na European Union's Copernicus Climate Service, ilifichua mabadiliko katika bahari, rangi ya kijani iko kwa kati ya asilimia 200 hadi 500 kuliko kawaida katika bahari ya Norway na Bahari ya Altantic kaskazini mwa Uingereza, hali iliyooneka Aprili 2023.

Lakini, rangi hiyo ilikuwa chini kwa asilimia 60 hadi 80 katika bahari ya magharibi ya Peninsula ya Iberia, lakini katika Bahari ya Mediterania kiwango cha rangi ya kijani ni asilimia 50 mpaka 100 juu kuliko ilivyokuwa awali. Vipimo hivyo vilichukuliwa kuanzia mwaka 1998-2020.

Aidha, uchambuzi wa BBC News wa halijoto ya bahari iliokusanywa na taasisi ya Copernicus, umefichua kuwa bahari duniani zinakabiliwa na ongezeko la joto, inayoonyesha kuwa joto baharini lilizidi kila siku katika mwaka uliopita wa 2023.

Miongo miwili ya kutumia setelaiti za NASA pamoja na wanasayansi kutoka Taasisi ya Teknolojia ya Massachusetts (MIT), iligundua kuwa zaidi ya nusu ya eneo la bahari duniani takribani asilimia 56 limebadilika rangi na kwamba ni sehemu kubwa kuliko ardhi yote duniani.

"Tunaona mabadiliko katika mabonde yote makubwa ya bahari mfano Pasifiki, Atlantiki na Hindi, haya ni mabadiliko makubwa ya kimataifa ambayo tunayaona," anasema B B Cael, mwanasayansi kutoka National Oceanography Centre huko Southampton, Uingereza.

Anasema hii inathibitisha nadharia katika ripoti ya awali ya Stephanie Dutkiewicz, mwanasayansi wa bahari kutoka Taasisi ya MIT na Kituo cha Global Change Science, aliyeripoti uwepo wa hali hiyo.

Mwaka 2019, Dutkiewicz akitumia kompyuta alitabiri mabadiliko ya baadaye katika rangi ya bahari, hata hivyo, ilikuwa vigumu kubainisha ikiwa hilo lilitokana na mabadiliko ya hali ya hewa au mifumo ya kawaida baharini.

"Ni vigumu kusema ikiwa mabadiliko haya yanatokana na hali ya hewa au la," anasema Dutkiewicz.

Utafiti wa Cael, ambao uliongeza data ya setilaiti, ulipanua wigo zaidi. Dutkiewicz, ambaye pia alifanya kazi katika utafiti wa Cael, anasema ripoti ya hivi karibuni inathibitisha utabiri wake.

"Vipimo vya satelaiti vinaendana na kile kinachoonekana kwenye taarifa yake," anasema na kuongeza "Kwa hivyo, mabadiliko tunayoyaona katika dunia yana uwezekano ni kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na binadamu."

Athari za mabadiliko haya kwenye bahari zinaweza kuwa kubwa. Watafiti wengine wametabiri mabadiliko ya rangi yatahamia kaskazini kwa kasi ya karibu kilometa 35 (maili 21) kila muongo wakati joto linapoendelea kupanda na kwamba itasababisha mabadiliko kwa viumbe vidogo vya baharini hasa wanaokula phytoplankton, huku utajiri wa viumbe mbalimbali (spishi) ukitarajiwa kupungua.

Lakini kuongezeka kwa joto la bahari, na kusababisha athari zaidi katika chakula na samaki wanaotegemea viumbe hawa ni jambo linalohofiwa.

Rangi ya bahari haitobadilika kwa usiku moja ama ghafla, lakini mabadiliko haya yanafichua mwelekeo ambao unaonyesha kuakisi itakavyokuwa kadiri halijoto inavyoongezeka.

"Sio rangi yenyewe ambayo inatia wasiwasi," anasema Cael na kuongeza. "Kilicho muhimu ni kuwa mabadiliko ya rangi yanaakisi kubadilika mifumo ya ikolojia ya bahari." **BBC SWAHILI**

ELIMU

NA DK. REUBENI LUMBAGALA

# Kuboresha utaalamu kiafya kunavyoifanya Tanzania shamba darasa la sekta ya tiba

KUTOA huduma bora kwa wagonjwa kunategemea uwepo wa vitu vingi, lakini moja kubwa ni wataalamu wa kutosha wenye ujuzi, maarifa na weledi katika magonjwa mbalimbali yanayowasumbua wananchi.

Hata kama kuna vifaa vya kisasa kunapokosekana wataalamu wa kuwahudumia wagonjwa vifo hutokea, kwa wale wenye fedha, hulazimika kuvuka mipaka kutafuta matibabu, jambo linaloongeza gharama za matibabu kutokana na kugharamia nauli, chakula, malazi, wasindikizaji na matibabu.

Wakati huu serikali inatoa msukumo na kipaumbele sekta ya afya kwa kuboresha miundombinu, upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na wataalamu ili kuhakikisha huduma zinazotolewa zinakidhi vigezo vya kitaifa na kimataifa.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB), inatoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu wanaosomea kozi mbalimbali, ambapo miongoni mwao ni wanafunzi wa kozi za afya ili kuongeza wigo wa wataalamu wa afya watakaotumia maarifa, ujuzi na stadi mbalimbali katika kuwahudumia wananchi.

Katika eneo ambalo bado taifa halijawa na wataalamu wa kutosha ni kwenye ubingwa na ubingwa bobezi. Kutokana na uhaba wa wataalamu hawa, Rais Samia Suluhu Hassan, ameweka mkakati wa kutoa ufadhili wa masomo unaogharimu bilioni 10.9 ili Watanzania wengi waweze kusoma na hatimaye kupunguza upungufu mkubwa uliopo sasa.

Fedha hizi zimetengwa ili kuwezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi kupitia mradi wa Dk. Samia Super-Specialized Scholarship Programme kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Akifungua mkutano wa mwaka wa Chama cha Madaktari Bingwa na Magonjwa ya Ndani Tanzania (APHYTA) jijini Dar es Salaam, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu anaeleza: "Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa madaktari bingwa katika kuwaendeleza kitaaluma kupitia programu ambayo imetoa nafasi za ufadhili wa masomo ya ubingwa kwa mwaka wa masomo 2023/2024, kwa wanafunzi 1,109 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 582 ukilinganisha na mwaka wa masomo 2022/2023."



Daktari akihudumia mgonjwa wa moyo. **PICHA: MTANDAO**

Utoaji wa ufadhili wa masomo kwa madaktari bingwa na ubingwa bobezi ni njia bora inayohakikisha upatikanaji wa wataalamu wa uhakika kwa manufaa ya nchi yetu badala ya kutegemea wale wa kutoka nje kuja kutoa huduma kwenye hospitali au vituo na kliniki spesheli.

Ni jambo la muhimu kwa taifa kujitosheleza kwa wataalamu wake wa ndani ili kuwa na uhakika wa huduma bora, hivyo basi, uwekezaji huo mkubwa wenye lengo la kuhakikisha nchi inakuwa na wataalamu mabingwa pia wenye ubingwa bobezi katika eneo la magonjwa yasiyoambukiza ni jambo la kupongezwa lakini vijana na wataalamu kuchukua hatua kwa kusoma.

Wataalamu hawa watakapohitimu masomo yao, watakuwa na jukumu la kutumia elimu waliyoipata katika kuwahudumia wananchi wa maeneo mbalimbali zilipo hospitali na vituo vy afya. Huduma watakazozitoa kwa wagonjwa zisaidie kuokoa maisha ya wananchi kwani kwa muda mrefu Tanzania imekuwa na upungufu mkubwa wa wataalamu hawa ambao ni muhimu kwa mustakabali wa afya na ustawi wa wananchi.

Kutokana na maboresha makubwa katika sekta ya afya, wapo wagonjwa kutoka nchi mbalimbali za Afrika wanaofuata huduma za tiba Tanzania. Kwa hiyo, uwepo wa madaktari hawa bingwa na ubingwa bobezi kunatoa fursa kwa sekta ya afya kuongeza mapato kutokana na kupokea wagonjwa wanaotoka nje ya mipaka wanaofuata huduma za matibabu kupitia utalii wa kimatibabu.

Kwa mfano, wagonjwa wa moyo kutoka Sierra Leone, watatibiwa Tanzania. Akizungumza wakati wageni kutoka Sierra Leone walipowasili katika Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI), Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, anasema:

> Fedha hizi zimetengwa ili kuwezesha wanafunzi 1,109 kwenye masomo ya ubingwa na ubingwa bobezi kupitia mradi wa Dk. Samia Super-Specialized Scholarship Programme...

"Tumepata wageni wenzetu kutoka Sierra Leone wamekuja kuona maendeleo haya kuanzia tulipoanza hadi sasa wamekuja kujifunza viongozi wetu wanavyotuongoza na kuwa na taasisi kama hii, vilevile utendaji kazi wa wahudumu wetu wa afya wanavyojituma ili wanapokwenda kuanzisha taasisi kwao wawe na uelewa wa kutosha."

Anaongeza kuwa wamekuja kujifunza ili kuleta wagonjwa kutoka Sierra Leone kutibiwa JKCI kwani wamejionea wenyewe kuwa watatibiwa kikamilifu na hii ni sehemu ya tiba utalii ambayo taifa linaiendeleza.

Ni jambo la faraja kuona Tanzania leo imekuwa shamba darasa katika sekta ya afya kwa mataifa mengine kuja kujifunza na kutibiwa pia. Haya yote yanatokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema na hata mataifa mengine yananufaika pia.

Kama anavyosema Waziri Ummy katika mkutano huo kuwa kupitia muundo mpya wa sekta ya afya, serikali itawatambua na pia kuwawekea mazingira mazuri madaktari wenye ubobezi katika maeneo mbalimbali ikiwamo wa masuala ya magonjwa ya ndani ambayo ni pamoja na maradhi ya figo, moyo na sukari.

Anawahakikishia wataalamu hao kuwa kuwatambua na kuwawekea mazingira bora madaktari bingwa na ubingwa bobezi ili kutoa huduma kwa wananchi ni muhimu kwani itawavutia kufanya kazi ndani ya nchi na katika maeneo mbalimbali hivyo kuwafikia wananchi wengi kwa huduma bora za kimataifa. Ikumbukwe kuwa moja ya vipaumbele sita vya kisera vya sekta ya afya kwa mwaka 2024/2025 ni pamoja na raslimali watu.

Ikumbukwe hawa ni wataalamu wa afya ambao wizara imepanga kuwajengea uwezo kwa kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili kuendana na mazingira na mahitaji ya utoaji wa huduma bora za kiafya. Hivyo basi, madaktari wanahitaji kujengewa uwezo kwa kupata mafunzo yatakayowawezesha kuwa madaktari bingwa na bingwa bobezi kazi ikifanyika mara kwa mara.

***Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Maoni: 0620 800 462.***

ELIMU

NA NA SABATO KASIKA

# Kutamka, kuandika 'apana, akuna, amna' kunavyokichafua Kiswahili

• Watetezi wa lugha kuibadilisha jamii

KISWAHILI kinapigiwa chapuo ndani na nje ya nchi kuwa miongoni mwa lugha za mawasiliano katika mikutano ya kimataifa na pia kufundishia kuanzia elimu ya msingi hadi vyuo vya elimu ya juu.

Licha ya juhudi hizo, kuna walakini kuzungumza na kuandika Kiswahili zama hizi kumekuwa kwa kubananga au kuharibu. Kwa mfano wapo wanaosema 'mwimbo' badala ya wimbo 'naniliu' badala ya 'nanihii ...'

Udhaifu huo unawaibua wataalamu wanaoeleza kuwa wakati lugha ikipigiwa debe tatizo lipo kwa baadhi ya watumiaji wake, hasa kwenye sarufi makosa yanayoonekana kwenye kuzungumza na kuandika.

Mahenda Jagadi, Mwenyekiti wa Chama cha Sarufi ya Kiswahili Tanzania (CHASAKITA), anabainisha hayo hivi karibini, wakati wa uzinduzi wa chama hicho, unaofanyika Bagamoyo mkoani Pwani.

Katika uzinduzi huo uliohudhuriwa na wadau mbalimbali wa Kiswahili, Jagadi anataja baadhi ya maeneo ambayo sarufi ya Kiswahili imekuwa haizingatiwi na watumiaji wa lugha hiyo huku akitoa ufafanuzi.

Anakumbusha kuwa sarufi katika lugha inahusisha kupanga maneno na kuyatamka kwa ufasaha na kwamba katika Kiswahili imegawanyika kwenye makundi mbalimbali, lakini makuu ni manne ambayo ni matamshi, maana, miundo ya maneno na mpangilio wa maneno katika sentensi.

Jagadi, anafafanua kuwa sarufi ni nyanja katika lugha inayoshughulikia maumbo, sauti, mpangilio wa maneno kwenye tungo na maana sahihi za maneno.

Anatolea mfano sarufi matamshi (fonolojia), kuwa hushughulikia matamshi ya vitamkwa vya lugha na kwamba kanuni za lugha huelekeza namna ya kuvitamka, mpangilio wa vitamkwa katika neno ambao huwezi kubadilisha maana.

Anagusia pia sarufi ya maumbo (mofolojia), kwamba hushughulikia jinsi maneno yanavyoundwa na kazi yake katika sentensi. Mpangilio wa vitamkwa uliotofauti huwezi kupoteza au kutunza maana iliokusudiwa.

"Lakini kuna sarufi muundo (sintaksia) ambayo hushughulikia uchanganuzi wa mpangilio au mfuatano wa maneno katika sentensi au tungo na uhusiano wa vipashio vyake, hushughulika na kanuni za kupanga maneno katika mpangilio sahihi," anasema.

Mwenyekiti huyo anataja sarufi maana (semantiki), kwamba inashughulikia maana inayoonekana na isiyoonekana katika sentensi, na huchunguza muundo wa tungo ili kupata maana, hasa iliyofichika.

Yote hayo tunataka Watanzania wajue maana yake na jinsi ya kuyatumia, badala ya jinsi ilivyo sasa, akieleza kuwa watu hawazingatii sarufi ya lugha ya Kiswahili katika maeneo mbalimbali.

"Kuna baadhi ya maneno yanayotatiza katika sarufi ya Kiswahili, kwa mfano neno hamsini, mtu anatamka 'amsini,' hapana wapo waoinatamka au kuandika 'apana' au hakuna utasikia 'akuna' au kwenye hamna 'amna'," anafafanua.

Anasema, yapo maeneo mengi ambayo sarufi ya Kiswahili hazingatiwi, jambo ambalo limewafanya waanzishe chama ili kusaidia wanachi kuizingatia wakati wa kuandika na kuzungumza.

Mwenyekiti huyo anasema, sababu kubwa ya watu kutozingatia sarufi ya Kiswahili, ni uingizaji wa sauti za irabu na konsonati ambazo hazimo katika sarufi ya matamshi ya Kiswahili.

"Hivyo, tumeamua kuanzisha chama hiki ili nasi tutoe mchango katika kuelimisha umma wa kutambua na kuzingatia sarufi kama njia ya kuenzi lugha hii ya taifa," anasema.



Mwenyekiti Mahenda Jagadi, akizungumza katika uzinduzi wa CHASAKITA. **PICHA: SABATO KASIKA**

> Marian tunajisikia fahari kuona chama hiki kinazinduliwa hapa lakini ni fahari kuona makao makuu yapo hapa hapa, hivyo, hii ni fursa kwetu kuijua lugha hii vizuri.

### KUTOA ELIMU

Mwenyekiti huyo anasema, kwa kuwa wameshazindua chama hicho, kitakachofuata ni kusajili wanachama wapya kisha wataanza kutoa elimu kuhusu umuhimu wa sarufi ya Kiswahili kupitia warsha, semina na makongamano katika maeneo mbalimbali nchini.

Anasema, wanachama watakaosajiliwa na chama hicho, ni wale wanaosoma Kiswahili katika vyuo mbalimbali, na kwamba watatumia miezi michache kuzunguka mikoani kuwasijili, baada ya hapo wataanza, warsha, semina na makongamano kutoa elimu.

"Tumeanza kupata wanachama katika Chuo cha Marian na tunaendelea kutafuta wengine katika vyuo mbalimbali ili tusaidiane kuelimisha Watanzania wenzetu umuhimu wa kuzingatia sarufi ya Kiswahili," anasema.

Mkurugenzi wa Maendeleo na Matumizi ya Kiswahili kutoka Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA), Kulwa Kindija, yeye anavitaka vyama vya kutetea Kiswahili vitengenezewe shirikisho.

Kindija ambaye alikuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa chama hicho, anasema vikiwa na shirikisho, vinaweza kufanya kazi kwa ushirikiano na kusaidia kuipasha zaidi lugha hiyo ya taifa.

"Lakini ninaomba viongozi wa CHASAKITA, mnapofanya ziara zenu, mfike kwetu BAKITA ili mjifunze mambo mbalimbali kuhusu lugha hii ya Kiswahili," anasema Kindija.

Mhadhiri wa Kiswahili kutoka Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Kampasi ya Kivukoni Dar es Salaam, Dk. Ahmad Sovu, anasema anatamani vyama vya kutetea Kiswahili viendelee kuongezeka.

"Pamoja na hayo, nikumbushe wadau wa Kiswahili kuzingatia mambo kadhaa wakati wa tunapozungumza lugha hii kwamba, tusiichanganye na Kiingereza, kwani kufanya hivyo ni sawa na kuendelea kukiharibu," anasema Dk. Ahmad.

Dk. Sovu anasema, imekuwa ni kawaida kusikia baadhi ya watu wakiharibu kwa kukichanganya na maneno ya Kiingereza, na kwamba kwa mtindo, itakuwa ni vigumu jamii kuijua vizuri lugha hiyo.

Mwakilishi wa Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Marian Tuladega Tweve, yeye anawahimiza wanafunzi wa chuo hicho wanasoma Kiswahili kuzingatia lugha hiyo, kwa kuwa ina fursa zake ni nyingi.

Anasema kwa sasa kuna nchi nyingi duniani zinazohitaji kufundishwa, na kwamba ni muhimu wanafunzi wajitahidi kuijua vizuri ili iwe rahisi kupata nafasi ya kuifundisha kwa ufasaha.

"Lakini pia ushauri wangu mwingine kwenu ni kuwa, mtakapohitimu chuo, mjiunge na chama hiki ili muweze kusaidia jamii kuboresha lugha yetu taifa izungumzwe kwa ufasaha," anasema Tuladega.

Aidha, anasema amefarijika kuona chuo kuwa makao makuu ya CHASAKITA, na kwamba hatua hiyo inaweza kuwa chachu kwa wanafunzi kuendelea kutilia mkazo somo la Kiswahili.

"Marian tunajisikia fahari kuona chama hiki kinazinduliwa hapa lakini ni fahari kuona makao makuu yapo hapa hapa, hivyo, hii ni fursa kwetu kuijua lugha hii vizuri," anasema.



## HABARI DODOMA

# Wanachama NGOs waitwa kugombea uongozi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMATI ya kuratibu uchaguzi wa Baraza la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NACONGO) imetoa wito kwa viongozi na wanachama wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs) kujitokeza kugombea nafasi za uongozi wa baraza ngazi ya mkoa na uwakilishi wa makundi maalum kimataifa.

Wito huo umetolewa juzi jijini hapa na Mwenyekiti wa kamati ya mpito ya kuratibu uchaguzi wa Baraza la Taifa la NGOs, Christina Ruhinda, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uchaguzi huo.

Alisema kwa kufanya hivyo watakuwa wameleta maendeleo ya sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali nchini, kwamba washindi wanatarajiwa kuapishwa Juni 11 mwaka huu.

Alisema uchukuaji wa fomu za kugombea utaanza Juni 3 hadi 4, 2024, fomu zitarudishwa Juni 5 hadi 6 mwaka huu, uchakataji wa fomu utafanyika Juni 7 hadi 8, huku kampeni na upigaji kura, kutangaza matokeo na kuapisha washindi litafanyika Juni 11, mwaka huu.

Aidha, alieleza sifa za wagombea wa nafasi za uongozi pamoja na vigezo vya shirika kushiriki katika uchaguzi huo ikiwamo shirika liwe limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya NGOs Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania.

Alisema mchakato wa uchaguzi wa baraza ngazi ya mkoa utaenda sambamba na uchaguzi wa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, kimataifa na wawakilishi wa makundi maalum. Alitaja sifa za mgombea wa nafasi za uongozi kuwa anatakiwa awe kiongozi au mwanachama katika NGOs iliyosajiliwa chini ya Sheria ya NGOs na mwenye uzoefu na uelewa mpana wa sera, sheria, kanuni na miongozo ya NGOS.

Pia, awe Mtanzania isipokuwa kwa mwakilishi wa NGOs ya kimataifa lakini mwenye kibali cha kufanya kazi Tanzania.

Alisema pia awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 70, asiwe alishawahi kupatikana na makosa ya jinai, awe na elimu ya kidato cha nne au zaidi, awe na uwezo mzuri wa kuzungumza lugha ya Kiswahili na Kiingereza na awe na akili timamu.

"Vigezo vya shirika kushiriki katika uchaguzi liwe limesajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya NGOs, Sura ya 56 ya Sheria za Tanzania, liwe linatekeleza shughuli zake katika eneo au afua husika, liwe katika orodha ya Msajili Msaidizi wa Halmashauri au wilaya au mkoa husika, pia liwe linatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo inayosimamia NGOs, ikiwamo ulipaji wa ada na uwasilishaji wa taarifa na kila NGOs lililokidhi vigezo vilivyotajwa hapo juu," alisema Ruhinda.

Aidha, alieleza kuwa kamati wamejipanga kuhakikisha inapambana na kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi wa baraza ngazi ya mkoa na uwakilishi wa makundi maalum.

# DC awapa ujanja wafanyabiashara mkoani Singida kuepuka usumbufu

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

MKUU wa Wilaya ya Mkalama mkoani Singida, Moses Machali, amewaagiza wafanyabiashara wilayani hapa kuhakikisha wanakata leseni za biashara, ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha baraza la biashara ambacho kilihudhuriwa na wafanyabiashara mbalimbali pamoja na wakuu wa idara na vitengo kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.

"Suala la leseni za biashara ni suala la lazima, tukate leseni za biashara ili tusije kukutana na adhabu mbalimbali, lakini pia tulipe kodi na ushuru kwa maendeleo ya wilaya yetu na kwa taifa kwa ujumla," alisisitiza.

Aidha, Machali aliwataka wafanyabiashara kuhakikisha wanajiandikisha kupata namba ya kitambulisho cha taifa ili kuweza kupata leseni kwa ajili ya kufanya biashara pamoja na shughuli mbalimbali zinahitaji kitambulisho hicho.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Asia Messos, aliwaomba wafanyabiashara na wananchi kuwekeza katika kiwanda cha kuchakata nyanya kilichopo Kata ya Gumanga wilayani Mkalama.

"Ningependa kutoa wito kwa wafanyabiashara kuja kuwekeza katika kiwanda hiki, tayari tupo katika mpango wa kuweka mashine mpya za kisasa, wananchi, wafanyabiashara wote mnakaribishwa," alisema.

Wakati huo huo Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amezindua kliniki ya kusikiliza kero za wananchi ambayo itakuwa inafanyika siku ya Alhamisi ya kila wiki katika wilaya zote mkoani hapa.

Alisema ofisi yake itakuwa inafanya zoezi hilo kwa mwezi mara moja na watagawana na Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, kwenda kwenye kila halmashauri kwa ajili ya kusikiliza na kutatua kero za wananchi.

Alisema: "Tunapokaa hivi tukawasikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowasumbua basi tutakuwa tumefanya jambo kubwa la kuwarejeshea wananchi furaha iliyopotea kwa kuondoa kero zao zinazowasumbua kwa muda mrefu".



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Pindi Chana, akijadiliana jambo na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Dk. Eliezer Feleshi, walipokutana bungeni Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waziri Mkuu mstaafu kuongoza maombezi uchaguzi serikali mitaa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, John Malecela anatarajiwa kuongoza kongamano maalumu la maombi kuliombea taifa, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu pamoja na Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Kongamano hilo linatarajia kufanyika kesho, limeandaliwa na vijana kutoka Jimbo la Dodoma Kanisa la Revival Evangelist Assemblies of God Tanzania (REAGT), litafanyika katika viwanja vya kanisa hilo lililopo Mtera Wilaya ya Mpwapwa mkoani hapa.

Aidha, maombi mengine yakayofanyika ni kuwaoambea viongozi wakuu wa nchi akiwamo Rais Samia Suluhu Hassan, pamoja na amani iliyopo.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini wa Kanisa hilo, Mchungaji Jackson Madelemo, alisema katika kongamano hilo pia watashiriki viongozi wa serikali akiwamo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene.

"Wengine ni viongozi wa serikali na vyama vya siasa, maaskofu, wachungaji kutoka madhehebu ya dini mbalimbali na wananchi wanaoishi Mtera," alisema.

Mchungaji Madelemo, alisema kongamano hilo litatumika kuwaelimisha vijana kujua na umuhimu wa kulinda amani na maadili ya kiroho.

Alisema elimu hiyo itawasaidia kuepukana na mafundisho potofu yanayoweza kuhatarisha amani kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu.

"Pamoja na kumwombea Rais Samia na viongozi na uchaguzi pia kongamano litaombea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, vijiji na vitongoji utakaofanyika mwaka huu na ule wa uchaguzi mkuu, hivyo vijana wataelimishwa umuhimu wa kulinda amani iliyopo pia kushiriki kwenye uchaguzi huo," alisema.

Kadhalika, alisema mambo mengine ambayo yatakayotiliwa makazo katika kongamano hilo ni pamoja na kuwahimiza vijana kujitokeza katika kujiandikisha kwenye daftari ya kudumu la mpigakura, kupiga kura na kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali.

**HABARI MBEYA**



# RC aonya wanaohujumu shughuli za uhifadhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewatahadharisha baadhi ya watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya na madiwani wanaoshirikiana kuhujumu shughuli za uhifadhi kwa kupokea rushwa kutoka kwa wafugaji na kuwaruhusu kuingiza mifugo kwenye misitu iliyohifadhiwa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa tahadhari hiyo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha baraza la madiwani la halmashauri hiyo kilichokuwa na lengo la kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema baadhi ya viongozi hao wamekuwa wakihujumu hata jitihada za serikali za kupandisha hadhi baadhi ya misitu kutoka kusimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kwenda kuwa mapori ya akiba ili yasimamiwe na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA).

Alisema hali hiyo inasababisha kuongezeka kwa migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji na mamlaka za uhifadhi pamoja na kusababisha uharibifu wa mazingira hasa misitu.

"Unasikia baadhi ya madiwani wanashiriki kuhujumu misitu, unasikia diwani fulani anashiriki kuwauzia wafugaji misitu, mnategemea sisi viongozi wenzenu tuwafikirieje? Bahati nzuri mimi ni mjumbe wa kamati ya siasa ya mkoa," alisema Homera.

Hivyo, aliwataka viongozi hao kuacha mara moja tabia hiyo kwa maelezo kuwa watachukuliwa hatua kali zikiwamo za kisheria ili iwe fundisho kwa wengine wenye tabia za aina hiyo.

Alisema wameshaagiza kila kijiji kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuchungia mifugo na hivyo hakuna sababu ya migogoro ya ardhi kuendelea kushamiri wilayani humo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chunya, Ramadhani Shumbi, alisema wilaya hiyo ndiyo inayoongoza kwa kuwa na misitu mingi mkoani humo na kwamba wanatakiwa kuilinda kwa gharama yoyote.

Aliwataka watendaji wa wilaya hiyo wanaofanya hujuma hizo kuacha mara moja ili kuhakikisha misitu hiyo inaendelea kuwapo na kuwasaidia wananchi.

Alisema kutokana na uwepo wa misitu hiyo, waliamua kwenda kujifunza kwenye mikoa mingine namna ya kuvuna hewa ya ukaa ili na wao waanze kuivuna.

Alisema: "Tulikwenda kujifunza kwa wenzetu namna ya kuvuna hewa ya ukaa, kamati ya fedha ilikwenda na ikaleta majibu ambayo yamejadiliwa kwenye vikao mbalimbali, sasa tunaendelea na hatua mbalimbali hivyo hawa wanaotuhujumu hawatutendei haki".

Aliwataka watumishi wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanafanya kazi kwa maslahi ya wananchi wa wilaya hiyo ili kuhakikisha wananchi wanapata wanachostahili.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Ofisa Tawala wa wilaya hiyo, Semwano Mlawa, aliahidi kufuatilia shughuli mbalimbali za maendeleo.



Mmoja wa askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Mbeya, akizungumza na dereva wa basi linalofanya safari zake kati ya Jiji la Mbeya na Wilaya ya Chunya ambalo lilipata ajali katika Kijiji cha Rwanjilo, inadaiwa chanzo ni mashimo ya barabarani. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 32% wanaotibiwa mguu kifundo wanakatisha matibabu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 32 ya watoto wanaopatiwa matibabu ya mguu kifundo katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya wanadaiwa kukatisha matibabu, hivyo kuwasababishia ulemavu wa kudumu.

Msimamizi wa matibabu ya mguu kifundo kwa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Dk. Veronica Marishay aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akiwapatia matibabu baadhi ya watoto wenye tatizo hilo.

Veronica ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Tiba ya Viungo wa Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, alisema tatizo hilo linasababishwa na ukosefu wa elimu ya kutosha kwa wananchi kuhusu tatizo hilo.

Aliwataka wananchi wanaokwenda na watoto wao kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya matibabu ya tatizo hilo kuhakikisha wanakamilisha dozi ili kuwaepusha watoto wao na ulemavu wa kudumu.

"Kazi tunayokuwa tumeifanya ya kuwatibu hawa watoto inakuwa haina maana tena kwa sababu watoto wanarudi kwenye ulemavu wa kudumu, sasa niwaombe wazazi ambao wanawaleta watoto hapa wajitahidi kukamilisha matibabu mpaka mwisho," alisema Dk. Veronica.

Alisema kwenye matibabu ya tatizo hilo wanafadhiliwa na Shirika lisilokuwa la kiserikali la MDH kwa kushirikiana na taasisi ya kimarekani ya Miracle Feet na kwamba watoto wanaojitokeza kutibiwa wanatibiwa bila malipo.

Alisema tangu mwaka 2015 mpaka sasa wamewahudumia watoto 2,199 ambao walikuwa na tatizo hilo la mguu kifundo katika mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini huku katika Hospitali ya Kanda wakitibu watoto 646.

Alisema baadhi ya watoto hao wanaendelea na huduma ya matibabu huku baadhi yao wakiwa wamemaliza na kupona tatizo hilo na kwamba wale waliokatisha dozi wana hatari ya kupata ulemavu wa kudumu endapo hawatatibiwa mpaka wakafikisha zaidi ya miaka mitano. Baadhi ya wazazi na walezi ambao waliwapeleka watoto wao kupata matibabu ya tatizo hilo waliishukuru Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa kuanzisha matibabu hayo wakidai kuwa yatawasaidia watoto wao.

Mmoja wa wazazi hao, Rosa Anyighulile alisema tangu alipoanza kumpeleka mtoto wake kwenye matibabu hayo ameanza kuona mabadiliko makubwa kwa maelezo kuwa mguu wa mtoto wake umeanza kunyooka.

Alisema awali alikuwa haelewi kwamba kuna matibabu ya aina hiyo na alipopata taarifa hiyo aliwahi na kuanza matibabu ambayo yamemsaidia mpaka sasa anaendelea vizuri.

"Namshukuru Mungu matibabu haya yameanza kuleta matokeo kwa mwanangu, kabla ya kuanza kutibiwa mwanangu nilijua ni mlemavu wa kudumu lakini sasa nimeanza kuona mabadiliko, nawashukuru sana madaktari," alisema Rosa.

Naye Rehema Abdallah alisema kutokana na matibabu hayo kutolewa kwa ufadhili wa mashirika, wamepunguziwa gharama akidai kuwa gharama wanazotoa ni za kuandikisha pekee.

Alisema kwa maelezo wanayoyapata ni kwamba gharama ya matibabu hayo ni kubwa ambayo pengine wasingeweza kuyamudu kutokana na uchumi wao.

## Mmomonyoko wa maadili vijana Njombe waishtua CCM

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

JAMII mkoani Njombe imetakiwa kuchukuwa hatua za haraka ili kudhibiti tatizo la mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

Ushauri huo ulitolewa wilayani Wanging'ombe mkoani hapa na kada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Enock Kiswaga, wakati wa uzinduzi wa kitabu cha Kijiji cha Uhekule ambapo amechangia kwa kununua vitabu 13 vya zaidi ya shilingi milioni nne.

Kiswaga alisema suala la mmomonyoko wa maadili linapaswa kuanza kudhibitiwa kuanzia kwenye ngazi ya familia.

"Haya matokeo ya juu tunayoyaona sasa ni matokeo ya ngazi ya familia, hiki kitabu nimeona dibaji yake wamezungumzia jinsi mambo yalivyokuwa yanaendeshwa zamani na mambo yanavyoendeshwa sasa hivi," alisema Kiswaga.

Alisema jamii inapaswa kujifunza katika kitabu hicho kwa sababu kimeeleza hali ilivyo mbaya kuhusu mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe, Claudia Kitta, kwa niaba ya Mbunge wa Jimbo hilo, Dk. Festo Dugange alisema Uhekule kimekuwa kijiji cha mfano kwa kuandika kitabu wazo ambalo linafaa kuigwa na vijiji vingine.

"Jambo hili siyo dogo ni kubwa na ndiyo maana napongeza wote waliounga mkono kwa akili na nguvu zao na mwendelee kuwa mfano kwa ajili ya kukuza historia ya nchi yetu kwa ujumla," alisema Kitta.

Baadhi ya waandishi wa Kitabu hicho kilichoeleza masuala mbalimbali akiwamo Dk. Flown Mgani alisema changamoto waliyokutana nayo ni pamoja na kukosa ushirikiano wa kupata taarifa sahihi.

Alisema: "Wazee ni kama walikuwa hawatuelewi tunaowauliza kuhusu taarifa za tamaduni, wengine wanasema tunataka kuwauza, wengine wanasema tunataka kuwapeleka freemason".

Kwa upande wao wakazi wa Kijiji cha Uhekule akiwamo Winfrida Kilagwa alisema kitabu hicho kinawakumbusha kuenzi mila na tamaduni za kiafrika badala ya kuendekeza usasa ambao unaleta madhara hadi kwenye afya kwa kula vyakula hatarishi.

Kitabu hicho kimeandikwa kwa ushirikiano na wananchi wa Uhekule wanaoishi mikoa mbalimbali ikiwa ni kijiji cha kwanza mkoani Njombe kuandika kitabu chake chenye kumbukumbu ya historia.



## Mkuya ataja changamoto 3 zinazoikabili Wizara ya Fedha

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, amesema, licha ya mafanikio yaliopatikana mwaka wa fedha wa 2023/2024 katika wizara hiyo bado inakabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo wafanyabiashara kutokuwa waaminifu.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Alisema ingawa kumekuwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wasiowaaminifu.

Alisema wafanyabiashara hao hawatumii mashine ya kielektroniki na wananchi wengi hawana mwamko wa kudai risiti.

Alisema changamoto zingine ni upungufu mkubwa wa fedha za kigeni hususani Dola za Marekani hali iliyopelekea kuathiri biashara hasa kwa wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Aidha, alisema wizara yake inaendelea kuweka mikakati madhubuti ya kuzitatua changamoto hizo ikiwamo kutoa elimu ya kutoa na kudai risiti na kuimarisha upatikanaji wa fedha za kigeni kwa uhakika.

Alisema mwelekeo wa bajeti wa wizara yake imewekwa vipaumbele 14 ikiwamo kusimamia ukusanyaji wa mapato ya serikali, kusimamia na kutekeleza bajeti yenye kusimamia jinsia na kuandaa upembuzi yakinifu kuhusu uanzishaji wa soko la hisa pamoja na benki ya uwezeshaji.

Pia, alisema kuimarisha utoaji wa huduma kwa wafanyabiashara wadogo pamoja na ukusanyaji wa mapato katika masoko mapya, kuimarisha usimamizi wa sera na kada ya ununuzi na kuimarisha usimamizi wa mali za umma kwa kukamilisha mfumo wa ZGAMIS.

Hata hivyo alisema kwa mwaka wa fedha 2024/2025 wizara yake inatarajia kukusanya Sh. trilioni 4.9 makusanyo hayo sawa ni ongezeko la asilimia 77 ikilinganishwa na makadirio ya kukusanya Sh. trilioni 2.7 yaliopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2023/2024.



# ACT-Wazalendo yalia ongezeko deni la taifa

Na Mwandishi Wetu

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo Zanzibar, Ismail Jussa Ladhu, amesema kukua kwa deni la taifa kunaongeza mzigo kwa wananchi ambao ndiyo walipa kodi.

Amesema kwa sasa deni la serikali ni Sh. trilioni 1.3 likiwa ni ongezeko kutoka Sh. bilioni 150 lililokuwa mwaka 2020.

Aliyasema hayo alipokuwa akihutubia mkutano wa hadhara uliofanyika Uwanja wa Kivumbi Jimbo la Shauri Moyo Mkoa wa Mjini Magharib Unguja.

Alisema deni hilo linatokana na mikopo ya ndani jambo ambalo litaongeza mzigo mkubwa kwa serikali na wananchi ambao ndiyo walipakodi na kuongeza ukali wa maisha.

Aidha, alisema serikali lazima itathmini upya ongezeko la madeni ya ndani ili kunusuru ukali wa maisha kwa wananchi na wafanyabiashara ambao wanaongezewa kodi kwa malengo ya kupunguza kiwango cha bei.

Akizungumzia miradi ya ujenzi wa masoko ya Chuwini, Mwanakwerekwe na Jumbi, alisema mradi huo ulipaswa kusimamiwa na halmashauri au manispaa kwa sababu ndiyo wahusika kwa mujibu wa sheria lakini unasimamiwa na serikali.


Jussa alisema gharama za mradi huo zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 73 mpaka Sh. bilioni 102 sawa na ongezeko la asilimia 29 kutokana na harufu kubwa ya rushwa katika miradi hiyo.

"Kuna masoko haya matatu la Mwanakwerekwe, Jumbi na Chuwini, masoko ni kazi ya halmashauri na manispaa, vipi leo ghafla serikali imejiingiza katika ujenzi wa masoko, baada ya makandarasi kushindwa wakapewa kazi hizo askari wa vikosi," alihoji Jussa.

Jussa alisema uchunguzi waliofanya wamegundua kupanda kwa gharama za ujenzi wa masoko hayo kumetokana na vifaa vya ujenzi kununuliwa kwa bei ya udanganyifu.

Mjumbe wa Kamati Kuu wa chama hicho, Mansour Yussuf Himid, alisema malengo ya mapinduzi yalikuwa kuwaunganisha Wazanzibar kuondokana na vitendo vya ubaguzi.

Alisema hivi sasa kuna malalamiko ya watu kunyimwa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi na kubaguliwa katika ajira, jambo ambalo halikubaliki.



Waziri wa Biashara na Viwanda, Omar Said Shabani, akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani nje ya mji wa Zanzibar, wakati akijibu hoja za wajumbe wa baraza hilo waliochangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka wa fedha 2024/2025. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ataka utafiti kubaini kushuka uzalishaji karafuu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Mfenesini, Machano Othman Said, ameitaka Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda pamoja na Wizara ya Kilimo kufanya utafiti unaobainisha sababu za kushuka kwa uzalishaji wa karafuu na kushindwa kuongoza katika soko la dunia.

Akichangia makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Biashara na Viwanda, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, alisema uzalishaji wa karafuu umeshuka ambapo katika miaka ya 1980 Zanzibar ilikuwa ikiongoza duniani.

Alisema utafiti wa kina unapaswa kufanyika kujua sababu za kushuka kwa uzalishaji kwa sababu ipo hatari uzalishaji wa zao hilo ukashuka zaidi.

Mwakilishi wa Mtoni, Hussein Ibrahim Makungu, alishangazwa na kushuka kwa uzalishaji wa karafuu visiwani Zanzibar, huku upande wa Tanzania Bara zao hilo likistawi vizuri.

Makungu aliitaka wizara kuitangaza karafuu ya Zanzibar ambayo itaweza kutambuliwa katika masoko yote duniani ili kuepuka kupoteza ubora na umaarufu wake.

"Wakati umefika kwa Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) kuja na mikakati ambayo itaitambulisha karafuu ya Zanzibar ubora wake popote duniani...nilikuwa Uingereza nikaomba karafuu nikaletewa nikaambiwa hiyo imetoka Pemba na niliibaini kutokana na ladha yake bora," alisema.

Mwakilishi wa Mtambwe, Dk. Mohamed Ali Suleiman, aliitaka ZSTC kuhakikisha linazalisha miche ya mikarafuu yenye ubora wa hali ya juu kwa ajili ya kuwapatia wakulima.

Akiwasilisha bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Biashara Maendeleo ya Viwanda, Waziri wa Wizara hiyo, Omar Said Shaban alisema Shirika la Biashara Zanzibar katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2024 lilitarajia kununua tani 4,380 za karafuu kavu kwa Sh.bilioni 60.4.

Alisema hadi kufikia Machi 2024, lilinunua tani 3,298.8 za karafuu kavu kutoka kwa wakulima kwa Sh.bilioni 47.5 ambazo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mwaka mzima.

"Shirika limenunua kilo moja ya karafuu kwa bei ya Sh. 15,000 kwa daraja la kwanza, daraja pili Sh. 13,500, daraja la tatu Sh. 12,500 na mpeta Sh. 7,000 kutoka kwa mwananchi," alisema.

Alisema shirika lilikadiria kununua tani 786 za makonyo kwa Sh. bilioni 1.17 na hadi kufikia Machi 2024, shirika lilinunua tani 627.6 za makonyo kwa Sh. milioni 941.4 sawa na asilimia 79.8 ya makadirio kwa miezi tisa.

Aidha, alisema ununuzi wa karafuu pamoja na makonyo yamepungua kutokana na msimu kuwa mdogo kinyume na matarajio.

Alisema shirika limefanikiwa kuuza karafuu nje ya nchi kwa bei ya Dola za Marekani 8,500 kwa tani moja, makonyo yameuzwa kwa bei ya Dola za Marekani 850 kwa tani moja.

Hata hivyo alisema, shirika liliuza nje ya nchi tani 3,190 za karafuu na makonyo tani 694.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ARTHUR PAUL MOSHA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya TOYOTA NOAH yenye usajili namba T 394 DMH, CHASSIS NAMBA: AZR603012985 na ENGINE NAMBA: 1AZ5367254. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/KIN/111674/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

EVARIST MDOKO TESHA anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya NISSAN DATSUN yenye usajili namba T159 ATX, CHASSIS NAMBA: GD21438520 na ENGINE NAMBA: NA1601521100. Kwa yeyote atakaeiona taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

PHQ/DAR/UBU/104649/2024

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**
**PHOTO**
**M/S GRACE GREEN MASHAKA**

By this deed,GRACE GREEN MASHAKA of Dar es Salaam,do hereby declare that the names GRACE GREEN MASHAKA,GRACE MASHAKA & GRACE GOLIN NTANGALA are mine and that they have been used interchangeably in lieu thereof I was born and named GRACE MASHAKA GOLINI NTANGALA whereas the name was erroneously written with GOLLIN instead of GREEN whereas I do hereby assume and adopt the name GRACE GREEN MASHAKA.
AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all material times hereinafter in all records,deeds and transactions and upon all occasions whatever use and sign the name GRACE GREEN MASHAKA make as my name.
AND I HEREBY AUTHORISE and request all persons to designate and address me by such name of GRACE GREEN MASHAKA.
I,the said GRACE GREEN MASHAKA make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of Oaths (Judicial Proceedings) and statutory Declaration Act.1966.
In witness whereof,I have hereunto set my hand this 07th day of SEPTEMBER,2021.




## KUPOTEA KWA CHETI



**ISRAEL ALBERT NGOWI** ANATANGAZA KUPOTEA KWA CHETI CHAKE CHA KIDATO CHA NNE CHENYE INDEX NAMBA S0308/0125/2014 KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI MWAKA 2014 KATIKA SHULE YA SEKONDARI YA ENABOISHU ILIYOKO ARUSHA.
KWA YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI .
**TAARIFA ARU/ARU/RB/773781/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**COSTANSIA PROSPER NGOWI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE(FORM 4) CHENYE NAMBA ZA USAJILI s1420-0046-2021,KUTOKA SHULE YA SEKONDARI YA KAYUKI(KAYUKI SECONDARY SCHOOL) RUNGWE MKOA WA MBEYA MWAKA2021.
KWA YOYOTE ATAKAEKIONA ATOE TAAFIFA KITUO CHA POLISI.
**TAARIFA YA POLISI:PHQ/MBE/MBE/15484/2024.**

## TANGAZO/ NOTISI YA MNADA WA HADHARA

**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTD** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED**, tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyo onyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya Siku saba (7) kama marudio ya tangazo na siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | HONESTY HENRY MINDE | AGUSTINE HENRY MINDE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | YOMBO VITUKA BARABARA YA MWINYI, MANISPAA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 18/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA NNE ASUBUHI NA KUENDELEA (*marudio ya tangazo*) |
| 2 | ENEA GODFREY BASAYA | GODFREY DAUDI BASAYA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | MBAGALA KWA NYOKA ,MANISPAA YA TEMEKE, DAR ES SALAAM | 26/06/2024 NA KUENDELEA KUANZIA SAA MBILI ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindi wa mnada ata lazimika kulipa malipo yasiyo pungua 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hatimiliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa bank (eviction) niza mnunuzi.
5. Mnunuzia akishindwa kutimiza sharti mojawapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**
**LEHALEL GROUP OF COMPANY LTDP.O.Box 68172**
**Dar es Salaam, Tanzania**
**Tel: 0620 848 565/ 0714 598 559**
**Email: lehalelglc@gmail.com**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GRACE CHRISTIAN OLOMI** anatangaza kupotea kwa kadi ya guta yenye USAJILI NAMBA: MC 490 DAY, CHASSIS NAMBA: LATZDMZY4M5931589 na ENGINE NAMBA: M5160735. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DOD/DOD/21424/2024**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO.7959 OF 2024**
**IN the Matter of the late:**
**FRANK SEVERINE MWALUKO**

**By 1.DEOGRATIUS SEVELINI MSIWE**
**2.............................................**


ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above- named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 13 day of june2024.
Dated at Morogoro this 03 day of june 2024.

.....................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

**CHANGE OF NAME BY DEED POLL**
**PHOTO**
**M/S GRACE GREEN MASHAKA**

By this deed,GRACE GREEN MASHAKA of Dar es Salaam,do hereby declare that the names GRACE GREEN MASHAKA,GRACE MASHAKA & GRACE GOLIN NTANGALA are mine and that they have been used interchangeably in lieu thereof I was born and named GRACE MASHAKA GOLINI NTANGALA whereas the name was erroneously written with GOLLIN instead of GREEN whereas I do hereby assume and adopt the name GRACE GREEN MASHAKA.
AND IN PURSUANCE of such change of name as aforesaid I hereby declare that I shall at all material times hereinafter in all records,deeds and transactions and upon all occasions whatever use and sign the name GRACE GREEN MASHAKA make as my name.
AND I HEREBY AUTHORISE and request all persons to designate and address me by such name of GRACE GREEN MASHAKA.
I,the said GRACE GREEN MASHAKA make this declaration conscientiously believing the same to be true in accordance with the provisions of Oaths (Judicial Proceedings) and statutory Declaration Act.1966.
In witness whereof,I have hereunto set my hand this 07th day of SEPTEMBER,2021.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
10.06.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe 11.06.2024 hadi 16.06.2024 kampuni ya CEVA Interfreight itasafirisha malori tupu yenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Bandari ya Dar es salaam, gari hilo lenye namba za usajili.

   **NRB97300 / NRB54202**
   **DSOOTG GP / NRB53910**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 28.0 Upana - mita 4.30 Kimo - mita 4.60**
3. Njia itakayotumika: Mzenga hadi Bandari ya Dar Es Salaam kupitia Barabara ya Morogoro, gari litasafiri muda wa mchana (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470 DODOMA,
10.06.2024

## TAARIFA KWA UMMA

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumatano tarehe 12-06-2024 hadi 14-06-2024 kampuni ya Mainline Carriers Ltd itasafirisha Mizigo wenye vipimo vikubwa kutoka Dar-Es-Salaam Port kuelekea Kilombero kupitia Mikumi, gari hizo zina namba za usajili:

**T 899 DSD / T 572 EAZ**
**T 972 EDR / T 879 EAU**

Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
**Urefu - mita 25.00**
**Upana - mita 4.35**
**Kimo - mita 5.20**

2. Njia itakayotumika: Dar-Es-Salaam, hadi Kilombero kupitia Mikumi, gari itasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

## KUPOTEA KWA VYETI



**WAZIRI ABDALLAH BONIFACE** anatangaza kupotea kwa TRANSCRIPT na CHETI CHA CHUO vyenye usajili namba SN 0192/0055/2016 vilivyotolewa na ST. GASPAR COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DOD/DOD/21486/2024**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701***

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Mpango polisi Kenya kwenda Haiti karibuni kukamilika

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto, amesema polisi wa taifa hilo wanatarajiwa kupelekwa nchini Haiti kukabiliana na magenge ya uhalifu ndani ya siku chache zijazo, licha ya pingamizi za mahakama ambazo zilichelewesha mchakato huo.

Kenya imekubali kuongoza kikosi kinachoungwa mkono na Umoja wa Mataifa kulinda taifa hilo la Caribbean, linalokumbwa na machafuko, umaskini na ukosefu wa uthabiti wa kisiasa.

Taifa hilo la Afrika Mashariki linapanga kupeleka maofisa wa polisi 1,000 kwa ajili ya operesheni hiyo pamoja na polisi wengine kutoka nchi nyingine kadhaa.

"Wananchi wa Haiti labda wanasubiri, kwa neema ya Mungu, labda kufikia wiki ijayo au itakayofuata, tutatuma maofisa wetu wa polisi kurejesha amani," Rais Ruto alisema katika hotuba wakati wa ziara katikati mwa Kenya.

Azimio la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa mwezi Oktoba mwaka jana liliidhinisha kupelekwa kwa kikosi hicho lakini mahakama ya Kenya mwezi Januari ilichelewesha mchakato huo.

Mahakama ilisema serikali haikuwa na mamlaka ya kupeleka maofisa wa polisi nje ya nchi bila makubaliano ya awali.

Lakini chama kidogo cha upinzani nchini Kenya kiliwasilisha kesi mpya kujaribu kuzuia mchakato huo, huku Mahakama Kuu ya Kenya ikitazamiwa kusikiliza kesi hiyo Juni 12, mwaka huu.



Tofauti na Kenya, nchi nyingine ambazo zilielezea nia ya kujiunga na kikosi hicho ni pamoja na Benin, Bahamas, Bangladesh, Barbados na Chad. **VOA**

# Misri, Qatar watishia kufukuza, kuwakamata viongozi Hamas

**DOHA,** Qatar

JARIDA la 'Wall Street' limesema kuwa Qatar na Misri hivi karibuni zimewaarifu viongozi wa Hamas kwamba huenda wakakabiliwa na uwezekano wa kukamatwa, kuzuiwa kwa mali, kuwekewa vikwazo na hata kufukuzwa kutoka Doha iwapo hawataunga mkono makubaliano ya kukomesha mzozo kati yao na Israel.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kwa kuzingatia maoni ya viongozi wanaosemekana kuhusika kwa kina katika mazungumzo haya, wanasema kuwa vitisho dhidi ya viongozi wa Hamas ni ombi kutoka kwa utawala wa Biden.

**Wanajua kwamba Qatar haina budi ila kuwafukuza viongozi wa Hamas ikiwa Marekani itawataka wafanye hivyo.**

Mkuu wa ofisi ya kisiasa ya Hamas, Ismail Haniyeh, ambaye yuko Qatar, alisema kuwa hawatakubali makubaliano ambayo hayakidhi matakwa ya kundi hilo na ambayo hayatoi hakikisho la kumalizika kwa vita.

Katika makala iliyoandikwa na mwandishi wa Mashariki ya Kati wa Jarida la Wall Street, Samar Saeed, aliongeza kuwa Hamas wiki hii ilipinga vikali pendekezo la hivi karibuni la kusitisha mapigano.

Jarida hilo lilisema kuwa tofauti kidogo ya maneno imekuwa kitovu cha mazungumzo, haswa baada ya Netanyahu kujibu hotuba ya Biden na kusisitiza kwamba vita haipaswi kumalizika kabla ya nguvu ya kijeshi ya Hamas kusambaratishwa.

Mkurugenzi wa Shirika la Ujasusi la Marekani (CIA) William Burns pia aliwataka viongozi wa Qatar na Misri kumfahamisha kiongozi wa Hamas Ismail Haniyeh kwamba wapatanishi wa kimataifa watathibitisha kuanza kwa mazungumzo kamili ya kusitisha mapigano.

Pia alieleza kuwa hatua hiyo itaanza katika wiki ya tatu ya awamu ya kwanza ya mazungumzo ya kusitisha mapigano na kufikia masharti ya kudumu ya mzozo huo ifikapo wiki ya tano, kwa mujibu wa jarida hilo.

Aidha, jarida hilo liliongeza kuwa, Haniyeh hakutikiswa na vitisho hivyo huku akisisitiza kuwa Israel inapaswa kutoa ahadi ya maandishi ya usitishaji vita wa kudumu hasa baada ya kauli ya Netanyahu kwamba hatakubali kusitishwa kwa mapigano hayo.

"Wanajua kwamba Qatar haina budi ila kuwafukuza viongozi wa Hamas ikiwa Marekani itawataka wafanye hivyo," ofisa aliyefuatilia kwa karibu mazungumzo hayo alinukuliwa akisema. **BBC**



Kansela wa Shirikisho la Ujerumani, Olaf Scholz, akipiga kura yake katika kituo cha kupigia kura huko Potsdam, Ujerumani, juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Emmanuel Macron avunja Bunge Ufaransa



**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron amesema ameamua kuvunja Bunge la taifa hilo na kuitisha uchaguzi baada ya chama chake kushindwa kwa kiasi kikubwa katika uchaguzi wa Bunge la Ulaya.

Akilihutubia taifa jana akiwa katika makazi ya rais jijini Paris, Macron alisema ameamua kurejesha chaguo la hatima ya bunge kupitia kura kwa kuvunja Bunge la Taifa, kwamba uchaguzi utafanyika kwa awamu mbili Juni 30 na Julai 7, mwaka huu.

Ilielezwa kwamba hatua hiyo ni baada ya duru kutoka Ufaransa kuonyesha chama cha mrengo wa kulia cha National Rally kiko mbele zaidi katika uchaguzi wa bunge wa Umoja wa Ulaya, na kuwashinda washirika wa Macron wanaounga mkono Ulaya.

"Nitatia saini katika muda mfupi agizo la kuitisha uchaguzi wa wabunge ambao utafanyika Juni 30 kwa duru ya kwanza na Julai 7 kwa duru ya pili," alisema Rais Macron.

Wakati wa hotuba yake, rais alikumbusha kwamba daima amezingatia kwamba Ulaya iliyoungana, yenye nguvu na huru ni hali ambayo hawezi kuitupilia mbali. Na kwamba kuongezeka kwa wahafidhina na kambi za mrengo mkali wa kulia, ni hatari kwa taifa hilo na umoja wa Ulaya kwa ujumla.

"Haki iliyokithiri ni ufukara wa Wafaransa na kushusha hadhi ya nchi yetu. Kwa hivyo, mwisho wa siku hii, sitaweza kutenda kana kwamba hakuna kilichotokea. Katika hali hii ni homa ambayo imeshika kasi juu ya mijadala ya umma na bunge katika nchi yetu katika miaka ya hivi karibuni.

"Ugonjwa ambao najua unawapa wasiwasi wakati mwingine huwashtua na ambao sitaki kuacha kukabiliana nao," alisema Rais Macron.

Wakati huo huo, nchini Ujerumani muungano wa Scholz umepata pigo kubwa katika uchaguzi wa bunge la Ulaya. Matokeo ya awali ya bunge yakionesha muungano wa Kansela wa Ujerumani Olaf Scholz umeshindwa, huku vyama vyote vitatu katika serikali yake vikiwa nyuma ya vile vya kihafidhina na mrengo mkali wa kulia.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Chama cha Social Democrats (SPD) cha Scholz kimepata matokeo mabaya zaidi katika historia kwa asilimia 14, kikiwa cha tatu nyuma ya chama cha siasa kali za mrengo wa kulia cha Alternative für Deustchland (AfD) kilichopata karibu asilimia 16, na nyuma pia ya kambi ya kihafidhina ya CDU, CSU kwa asilimia 30.

Vile vile, ilielezwa kuwa washirika wa muungano wa SPD, walinzi wa mazingira 'The Greens' wamepata asilimia 12 huku chama cha kiliberali cha FDP kikipata asilimia tano. **RFI**

# ADEBAYOR AWINDWA

Na Adam Fungamwango

KLABU ya Singida Black Stars, imeanza harakati za kukisuka upya kikosi chake na tayari wapo kwenye mchakato wa kumsajili winga raia wa Niger, Victorien Adebayor.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya Singida Black Stars zinasema kuwa uongozi wa timu hiyo umegonga hodi kwa wawakilishi wa mchezaji huyo wakiamini ni mchezaji mkubwa na atawasaidia kwenye kikosi hicho kinachohitaji kucheza michuano ya kimataifa msimu ujao.

Adebayor, si jina geni hapa nchini kwani alikuja na kikosi cha US Gendamarie ya Niger wakati wa michuano ya Kombe la Shirikisho kucheza dhidi ya Simba na klabu hiyo kuonyesha nia ya kumsajili kwa misimu miwili mfululizo, mashabiki wa timu hiyo wakiaminishwa hivyo, lakini hadi leo imekuwa kimya.

**Kwa sasa mchezaji huyo anakipiga kwenye klabu ya AS GNN ya Niger, akitokea Amazulu FC ya Afrika Kusini ambayo ilimsajili kutoka RS Berkane ya Morocco, iliyoipiku Simba katika dau la usajili kutoka US Gendamarie.**

"Hatutanii, tumeamua kufanya usajili mkubwa, tumegundua ukiwa na wachezaji bora ni rahisi tu kupata tiketi ya kucheza mechi za kimataifa. Angalia Coastal Union, mpaka mzunguko wa kwanza ilikuwa haieleweki, lakini ilipofanya usajili bora tu dirisha dogo leo hii imepata tiketi ya kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, hii imetutia hamu sana ya kufanya usajili wa wachezaji wazuri," alisema mtoa taarifa ndani ya klabu hiyo.

Mbali na mchezaji huyo, timu hiyo ambayo tayari imeshaachana na jina la Ihefu, kwa mujibu wa mtoa taarifa pia iko katika hatua za mwisho kupata saini za wachezaji, Hervy Ossete, kiungo mkabaji kutoka Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, beki wa kushoto raia wa Ghana, Ibrahim Imoro kutoka Al Hilal ya Sudan na golikipa Mohamed Kamara raia wa Sierra Leone anayeichezea Horoya ya Guinea.






Mwenyekiti wa Utamaduni mkoani Simiyu, Buhimila Shala (wa tatu kushoto), akiongoza uzinduzi wa Tamasha la Utamaduni na Utalii Kanda ya Ziwa, kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kilimanjaro One Travel and Tours, Christina Emmanuel ambaye ni mwandaaji wa tamasha hilo, Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Mohamed Hatibu, Mkurugenzi wa Ukaguzi na Maendeleo ya Sanaa kutoka Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Edward Buganga, Ofisa Masoko kutoka Bodi ya Utalii Tanzania, Nassor Garamatatu na Ofisa Utamaduni wa Wilaya ya Bariadi DC, Yohana Misese. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Mashujaa yamaliza usajili, kuweka kambi Zenji*

Na Mwandishi Wetu

BAADA ya kunusurika kushuka daraja au kwenda katika mechi za mchujo 'play off' katika mchezo wa mwisho wa Ligi Kuu, klabu ya Mashujaa FC imeonekana kujipanga vyema kuelekea msimu ujao baada ya kukamilisha usajili wa wachezaji iliokuwa inawahitaji, huku ikitarajiwa kuanza maandalizi ya msimu mpya Juni 28 visiwani Zanzibar.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo ambaye hakutaka jina lake liwekwe gazetini kwa madai si msemaji rasmi wa timu alibainisha kuwa timu hiyo imekamilisha usajili kwa asilimia 100 na kinachosubiriwa ni kutangazwa rasmi, huku akisema kikosi kitapiga kambi yake mjini Zanzibar kujiandaa na msimu wa 2023/24.

"Ligi ilikuwa ngumu hadi mzunguko wa kwanza unamalizika tulikuwa na pointi nane, tukafanya mabadiliko, tukasajili wachezaji 13, tukawaacha 21 tukamaliza na pointi 35, tunamshukuru Mungu," alisema kiongozi huyo.

Kuhusu maandalizi ya msimu ujao alisema yamekamilika na kwa sasa wanasubiri siku ifike waende kuweka kambi Zanzibar.

"Tarehe 28 mwezi huu tunategemea kuanza maandalizi ya msimu ujao 'pre-season' mjini Zanzibar.

Kuhusu maboresho, mwalimu ameshatoa ripoti yake, tumeifanyia kazi, tumeongeza baadhi ya wachezaji, tutawatangaza rasmi tutakapokuwa tayari kufanya hivyo. Kwa kikosi cha msimu ujao malengo yetu ni kumaliza kwenye nafasi nne za juu," alisema.

Mashujaa, yenye maskani yake Kigoma, ilimaliza ligi msimu uliomalizika ikiwa kwenye nafasi ya nane kwenye msimamo, ikicheza mechi 30 na kushinda michezo tisa, ilitoka sare michezo nane na kufungwa michezo 13.

# Matumaini nafasi ya pili KMKM SC yazidi kupotea

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MATUMAINI ya KMKM SC kumaliza ligi katika nafasi ya pili yamezidi kufifia baada ya juzi kukubali kipigo cha mabao 2-1 kutoka kwa KVZ FC na kujikuta ikishuka mpaka nafasi ya tatu.

Ligi hiyo ya Zanzibar imebakisha michezo miwili kukamilisha msimu huu. Zimamoto SC wamepanda mpaka nafasi ya pili baada ya kushinda mchezo wa juzi dhidi ya Chipukizi kwa mabao 2-0.

Katika msimamo wa Ligi hiyo, JKU SC anaendelea kuongoza akiwa na pointi 62, nafasi ya pili inashikwa na Zimamoto SC waliofikisha pointi 58 na KMKM yenyewe ina pointi 53 kwenye nafasi hiyo ya tatu.

Timu tatu za juu ukiondoa Zimamoto wenye michezo mitatu zote zimebakisha michezo miwili kumaliza msimu.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa Zimamoto SC, Mohmed Hilali alisema bado wapo katika mbio za ubingwa kwa kuwa wanayo nafasi ya kufanya hivyo.

Alisema kwa mujibu wa msimamo wa Ligi ulivyo bado wanaendelea na harakati zao za kuhakikisha hawapotezi mchezo wowote ulio mbele yao ili kufanikisha lengo lao.

Alisema mpaka sasa wanautofauti wa alama nne na vinara wa ligi hiyo huku wakiwa na faida ya michezo mitatu ambayo bado hawajacheza.

"Tupo katika mbio za ubingwa mpaka hatua ya mwisho, tunaangalia mechi zetu kwanza, tunataka kupambana tushinde zote huku tukimwombea mpinzani wetu apoteze hata moja tu," alisema Hilali.



Wachezaji wa KVZ mazoezini

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### TSYGANKOV AWANIWA

ARSENAL inamfuatilia kwa karibu winga wa Girona mwenye wa miaka 26 kutoka Ukraine, Viktor Tsygankov, ambaye anasakwa na AC Milan. ***(Sport)***

#### SESKO AGOMBEWA ENGLAND

CHELSEA ina imani kuwa inaweza kushindana na Arsenal katika harakati za kumsajili mshambuliaji wa Slovenia, Benjamin Sesko kutoka RB Leipzig mwenye miaka 21. ***(Standard)***

#### MAN U YASAKA NYOTA

KLABU ya Manchester United ina nia ya kumsajili beki wa Everton na England, Jarrad Branthwaite mwenye miaka 21, huku wakitafuta kuimarisha safu yao ya ulinzi. Beki wa Juventus na Brazil, Gleison Bremer mwenye miaka 27, na mlinzi wa Nice na Ufaransa Jean-Clair Todibo mwenye miaka 24, pia wanawindwa na klabu hiyo. ***(Football Insider)***

#### JADON SANCHO NA MAN U

MANCHESTER United ipo tayari kufanya mazungumzo na winga wa Uingereza Jadon Sancho mwenye miaka 24, kabla ya kuamua kuhusu mustakabali wake. Sancho aliisaidia Borussia Dortmund kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kujiunga nayo kwa mkopo kufuatia kutofautiana na Kocha wa United Erik ten Hag. ***(ESPN)***

#### WEST HAM YAMTAKA GARCIA

KLABU ya West Ham inajaribu kuzuia jaribio la Bayer Leverkusen kumsajili kiungo wa kati wa Girona na Hispania, Aleix Garcia mwenye umri wa miaka 26. ***(Guardian).***

#### ...YAMTAKA PIA JOTA SILVA

WEST Ham pia wanataka kumsajili winga wa Vitoria Guimaraes na Ureno, Jota Silva mwenye miaka 24. ***(Teamtalk)***

#### MKATABA WA KUDUMU

KLABU ya Tottenham inamwania, Djed Spence mwenye miaka 23 ili kumpa mkataba wa kudumu baada ya kufanya vizuri kwenye klabu ya Genoa aliyoichezea kwa mkopo msimu uliopita. ***(Fabrizio Romano)***

#### PARDEW AIVUTIA NEWCASTLE

KOCHA wa zamani wa Newcastle United na West Ham, Alan Pardew mwenye miaka 62, anasema amevutiwa na kazi ya kuinoa Burnley. ***(Talksport)***


#### ADARABIOYO HUYO CHELSEA

MLINZI wa Fulham, Tosin Adarabioyo mwenye miaka 26, amefanyiwa uchunguzi wa afya kabla ya kuhamia Chelsea. ***(Mail)***

#### DYBALA KUHAMIA ENGLAND

MSHAMBULIAJI wa AS Roma mwenye miaka 30, Paulo Dybala yuko tayari kuhamia Ligi Kuu England msimu huu. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MINTEH ATAKIWA LIVER

**LIVERPOOL,** England

**Newcastle inaweza ikalazimishwa kumuuza mapema katika dirisha la majira ya kiangazi ili...**

LIVERPOOL imeonesha nia ya kutaka kumsajili winga wa Newcastle United, Yankuba Minteh, kulingana na ripoti.

**Newcastle inaweza kulazimishwa kuuzwa mapema katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi ili kukidhi kanuni za faida na uendelevu za Ligi Kuu England pamoja na kufadhili biashara zao.**

Gazeti la Telegraph linadai kwamba Magpies hao wameamua kukubali bila kusita ofa ya karibu pauni milioni 40 kwa Minteh, ambaye alitumia msimu uliopita kwa mkopo Feyenoord.

Akiwa Feyenoord, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19 alisimamiwa na kusifiwa na kocha mkuu mpya wa Liverpool, Arne Slot.

Minteh alifunga mabao 11 na asisti sita katika kipindi chake cha mkopo cha mwaka mmoja nchini Uholanzi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Gambia pia anavutiwa na klabu za Italia na Ujerumani.

Minteh alisajiliwa kwa mara ya kwanza na Newcastle kutoka Odense ya Denmark majira ya joto yaliyopita kwa pauni milioni 6.5.

Wanaweza kumbadilisha haraka kwa faida na kutumia fedha hizo kuleta winga mpya ambapo nyota Jarrod Bowen, Michael Olise na Nico Williams wote wapo kwenye rada zao. Kumuuza Minteh pia kutafungua milango kwa Newcastle kuwabakisha wachezaji nyota Alexander Isak na Bruno Guimaraes.

Dakika 90 ziliripotiwa mapema mwaka huu kwamba Magpies wangependa kumuuza Guimaraes kuliko Isak, huku Arsenal na Manchester City wakiwa miongoni mwa timu zinazomtazama kiungo huyo wa Brazil.

Newcastle pia wamekabiliwa na pigo la ziada la kutoshiriki Europe msimu ujao, ambalo litapunguza kiwango cha juu cha mapato wanachoweza kupata katika kipindi cha kampeni na kupunguza hitaji lao la kuwa na kikosi kikubwa.

Liverpool, kwa upande wake, wanaanza marekebisho yao katika zama za baada ya Jurgen Klopp na watarejea Ligi ya Mabingwa msimu ujao wakiwa wamemaliza nafasi ya tatu kwenye Premier League.

Slot ameteuliwa kama kocha mkuu badala ya meneja kama sehemu ya urekebishaji wa klabu.

# MBAPPÉ AIKERA BAYERN




**MUNICH,** Ujerumani

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Max Eberl, amekemea kupanda kwa gharama za uhamisho kwa sasa, akisisitiza kwamba uhamisho wa Kylian Mbappe kwenda Real Madrid unaweza kuwa "msumari kwenye jeneza".

Mbappe alijiunga na Madrid kwa uhamisho wa bure kutoka Paris Saint-Germain msimu huu wa majira ya joto lakini pamoja na mshahara mkubwa, Mfaransa huyo pia inasemekana alikubali ada ya kusaini ya euro milioni 150.

Habari za makubaliano na Mbappe zilikuja kama mshtuko mkubwa kwa Eberl, ambaye alisisitiza kuwa haifanyi chochote isipokuwa kuharibu soko la uhamisho.

"Fedha zinaondoka sokoni," aliambia Suddeutsche Zeitung. "Hakuna klabu inayonufaika nayo. Wachezaji, familia, washauri, kila mtu anafaidika, lakini hakuna klabu.

"Hapo awali, ilikuwa ni kawaida kwamba angalau klabu zilinufaika. Fedha zilibaki kwenye mzunguko.

"Unaweza kuzidi kuwa mchoyo, lakini kila mwenye tamaa taratibu atakua msumari kwenye jeneza la soka, fedha zote zikiisha wakati fulani basi hatutakuwa na la kufanya.

"Fedha ni kubwa sana na wakati fulani unapata hisia kwamba itapasuka. Kwa hiyo wakati fulani itakuwa imejaa kupita kiasi na wakati fulani Saudi Arabia itakuja. Unapata hisia kwamba si halisi.

"Sitaki kushiriki katika suala zima, lakini bila shaka nataka pia kufanikiwa. Kama mtu anayehusika na michezo, pia nimekumbwa na shida hii."

# Real kugomea Klabu Bingwa ya Dunia

**MADRID,** Hispania

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema kwamba miamba hiyo ya Hispania ina nia ya kukataa mwaliko wa kushiriki michuano ya Kombe la Dunia la klabu litakalofanyika mwakani.

Michuano hiyo inatarajia kuongezeka kwa timu na kufanya jumla ziwe 32 zitakazocheza kwa muda wa wiki nne nchini Marekani baada ya msimu wa 2024/25 kumalizika.

Madrid ilitegemewa kuwa mmoja ya washiriki baada ya kushinda taji hilo kwa mara 5 katika miaka 9 iliyopita, lakini Ancelotti amethibitisha kwamba timu yake haitocheza kwenye mashindano hayo kwani FIFA haijatoa ofa yenye fedha za kutosha na anaamini kwamba timu nyingine zitafuata nyayo zao pia.

Ancelotti amesema kwamba, mechi moja tu ya Real Madrid ina thamani ya Euro milioni 20 ( zaidi ya shilingi bilioni 56.6) lakini FIFA wanataka kuipa klabu hiyo kiasi hicho cha pesa katika michezo yote ya michuano hiyo, hivyo wao kama timu wameona pesa hiyo haitoshi.

Maamuzi ya FIFA ya kuongeza timu na hivyo idadi ya mechi kuongezeka, yamekutana na vipingamizi kutoka kwa wadau mbalimbali wa soka wakiwamo wachezaji wenyewe na makocha wakidai kwamba haijaangalia hali ya kiafya ya wachezaji kutokana na kuongezeka kwa majukumu na wanaamini hii inaweza ikaua mpira wa miguu.





# *Tuchel basi tena Man U*

**MUNICH,** Ujerumani

KOCHA wa zamani wa Bayern Munich, Thomas Tuchel hayuko tena kwenye mbio za kuchukua nafasi ya Erik ten Hag pale Manchester United, kwa mujibu wa ESPN.

Baada ya kuondoka kwa Tuchel ndani ya Bayern, alipigiwa upatu kuwa mshindani mkuu kuchukua nafasi ya Ten Hag ikiwa mmiliki mwenza mpya wa United Sir Jim Ratcliffe ataamua kuachana na Mholanzi huyo msimu huu wa majira ya joto.

Tuchel hivi majuzi alikutana na maofisa wa United kujadili kazi hiyo kama ilivyofichuliwa kwa mara ya kwanza na Fabrizio Romano, mkufunzi huyo wa zamani wa Chelsea na Bayern sasa anatazamia kupumzika.

Kwa mujibu wa gazeti la Times Tuchel alimpigia simu Ratcliffe moja kwa moja.

Mauricio Pochettino, Kieran McKenna na Thomas Frank pia wamezungumzwa na United kama sehemu ya mchakato huo, ambao unatarajiwa kufikia hitimisho thabiti wiki hii.

Roberto De Zerbi, ambaye aliondoka Brighton & Hove Albion msimu huu wa joto, inaeleweka kuwa atawavutia pia.

Kwa upande wake, Ten Hag amekuwa akisisitiza mara kwa mara kuwa anaamini kuwa atasimamia msimu ujao, tayari amehusika katika mazungumzo ya uwezekano wa kuhama na mmiliki mpya.

## Yanga, Safari Champion kukipiga Juni 29

**Na Mwandishi Wetu**

MABINGWA wa soka nchini, Yanga wameingia makubaliano na Kampuni ya bia nchini (TBL) kucheza mchezo maalum na kikosi cha Safari Champion Juni 29 kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

Ikumbukwe TBL iliendesha mashindano maalum ya kusaka vipaji na kuchagua wachezaji waliounda timu hiyo ya Safari Champion.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtendaji Mkuu wa Klabu ya Yanga, Andrew Ntime, alisema makubaliano hayo yatasaidia kuinua vipaji vya vijana ambao watazitumikia timu za Taifa hapo baadaye.

"Hii ni fursa ya pekee kwetu kuingia makubaliano na kampuni hii katika kuhakikisha tunaibua vipaji vya vijana ambao hapo baadaye watazitumikia timu za Taifa," alisema Mtime.

Kwa upande wake Meneja wa chapa wa TBL, Pamela Kikalu, alisema timu hiyo ya Safari Champion ina jumla ya wachezaji 22 ambao wamepatikana katika mikoa minne ya Tanzania Bara, kupitia mchakato wao uliaoanza mwezi Agosti mwaka jana.

"Mchakato huu ulianza tangu mwezi Agosti kwa kukusanya vijana zaidi ya 1,000 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara ambao tuliwafanyia mchujo na kupata idadi hii," alisema Kikalu.

Alisema mbali na tamasha hilo vile vile kutakuwa na burudani zitakazotolewa na wasanii Harmonize wa Tanzania pamoja na Koffi Olomide kutoka Kongo.

# SERIKALI: TUTAJENGA VIWANJA KWA WAKATI

**Na Shufaa Lymo**

SERIKALI imeahidi kuendelea kujenga viwanja mbalimbali hapa nchini na kukamilika kwa wakati kwa ajili ya mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika AFCON) yatakayofanyika katika nchi za Tanzania, Kenya na Uganda mwaka 2027.

**Akizungumza na wadau wa michezo juzi usiku jijini Dar es Salaam kwenye hafla ya utoaji tuzo za Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kwa wanamichezo waliofanOya vizuri mwaka 2023, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa, alisema viwanja hivyo vitakapokamilika vitatumika na timu zitakazokuja hapa nchini kwa ajili ya michuano hiyo ya AFCON.**

Alisema ni jambo la kujivunia kwa Tanzania kupata fursa ya kuandaa mashindano makubwa kama hayo ambayo kumetokana na juhudi za serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha nchi inafika mbali kupitia michezo.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi watengeneze viwanda ambavyo vitakuwa vinauza vifaa vya michezo kwa bei rahisi ili kila mtanzania aweze kuvinunua, pamoja na kuwasihi wazidi kuwekeza katika michezo kwani inajenga afya vile vile husaidia vijana wengi kupata ajira.

Katika hatua nyingine, Waziri Mkuu aliwapongeza wachezaji wote waliopata tuzo na kuwataka wale ambao hawajashinda wasikate tamaa na badala yake wajipange kwa ajili ya mwaka ujao.

"Nawapongeza wanamichezo wote walioshinda tuzo na kwa wale ambao mwaka huu hawajashinda, nafasi bado ipo mwakani, wapambane na kujituma kwenye michezo yao ili wawe kwenye nafasi ya kushinda tuzo," alisema.

Miongoni mwa tuzo zilizotolewa juzi ni tuzo za heshima ambazo ilitolewa kwa Waziri Mkuu pamoja na Mwenyekiti BMT. Azam Media ilipata tuzo ya mdhamini bora, pamoja na Benki ya NBC.

Kwa upande wa tuzo za wanamichezo bora wa kike shuleni na wanamichezo bora wa kiume zilikwenda kwa Happiness Fabian (Netiboli) na Agape Mwenda (Soka).

Tuzo za wanamichezo bora chipukizi wa kike na wa kiume zilikwenda kwa Winfrida Gerad (soka) pamoja na Romeo Asumbisye (kuogelea).

Vosta Isaya alipata tuzo ya mchezaji bora kwa upande wa watu wenye ulemavu kupitia mchezo wa tenisi huku tuzo ya mwanahabari bora wa kike ikienda kwa Fatma Chikawe (Azam Media) na Hussein Shafii (TBC). Pendo Njau aliibuka mshindi wa mwamuzi bora wa kike (ngumi) huku upande wa mwamuzi bora wa kiume akiwa Ahmed Arajiga (soka).

Kocha wa JKT Queens, Ester Chaburuma alipata tuzo ya kocha bora wa kike huku Antony Muingereza akiibuka kocha bora wa kiume kupitia riadha.

Timu ya JKT Queens iliweza kushinda tuzo ya timu bora ya wanawake, ambapo Yanga iliibuka kidedea kwa upande wa timu ya wanaume.

Huku timu bora ya Taifa ya Wanawake kriketi iliibuka na ushindi na upande wa wanaume ni Taifa Stars.

Mwanamichezo bora wa mwaka upande wa wanawake tuzo ilienda kwa Grace Joseph huku upande wa kiume tuzo hiyo ikienda kwa Yusuph Changarawe ambapo wote ni mabondia wa ngumi za ridhaa.



Wafanyakazi wa Standard Chartered na familia zao wakifanya mazoezi kabla ya kuanza kufanya usafi katika ufukwe wa Msasani jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Simba, Yanga kukutana

INATOKA UKURASA 24

nne.

Kama ilivyokuwa msimu uliopita ambapo mfumo wa kuwa na timu nne kwenye Ngao ya Jamii ulipoanza, ambapo Yanga iliyokuwa bingwa ilicheza dhidi ya Azam FC iliyokuwa mshindi wa tatu, Agosti 9, Simba iliyomaliza ya pili ilicheza dhidi ya Singida Fountain Gate, Agosti 10 katika mechi zilizopigwa kwa mtindo wa mtoano, na watani wa jadi hao wakakutana fainali Agosti 13, 2023 na Simba kutwaa Ngao hiyo kwa ushindi wa mikwaju ya penalti 3-1 baada ya kumaliza mchezo bila kufungana.

Michuano hiyo mwaka jana ilifanyika kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga.

Hata hivyo, katika taarifa yake TFF bado haijataja michuano hiyo itafanyika mkoa gani.

Mchezo wa Simba na Yanga utakuwa wa pili kwa mwaka huu timu hizo kukutana ambapo mara ya mwisho zilicheza Aprili 20 mwaka huu, Yanga ikishinda mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ukiwa mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Rekodi inaonyesha Yanga imeifunga Simba mechi zote mbili za Ligi Kuu msimu huu ambapo katika mechi ya mzunguko wa kwanza, iliyochezwa uwanja huo huo, Novemba 5 mwaka jana, iliibuka na ushindi mnono wa mabao 5-1.

## Taifa Stars kusaka pointi tatu kwa Zambia



Boniface Wambura

INATOKA UKURASA 24

mabao ya kufunga na kufungwa, huku Morocco ikiongoza kundi kwa pointi sita, baada ya Ijumaa iliyopita kuifunga Zambia mabao 2-1.

Iwapo timu yoyote leo kati ya Stars au Zambia itashinda, itafikisha pointi sita sawa na vinara, Morocco.

# Michezo

Jumanne Juni 11, 2024

Nipashe




Real kugomea Klabu Bingwa Dunia UKURASA 22



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akimkabidhi Tuzo ya Mwanamichezo Bora wa Kike wa mwaka, Bondia Grace Joseph kwenye hafla ya utoaji tuzo za Baraza la Michezo la Taifa (BMT) juzi usiku jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba, Yanga kukutana Ngao ya Jamii Agosti

**Na Adam Fungamwango**

## TFF yatangaza michezo hiyo itakayoshirikisha timu nne kuchezwa kuanzia...

SHIRIKISHO la Soka Tanzania (TFF) limetangaza michuano ya Ngao ya Jamii ikiwa ni ishara ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2024/2025 itachezwa kuanzia Agosti 8-12 huku Simba na Yanga zikicheza zenyewe kwa zenyewe.

**Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana mchana na TFF, michuano hiyo itakayoshirikisha timu nne, Simba, Yanga, Azam na Coastal Union itafanyika kwa siku tano kuanzia Agosti 8.**



Ingawa TFF haijatoa ratiba yake, lakini kanuni ya michuano hiyo inaelekeza bingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara atacheza na mshindi wa tatu wa ligi hiyo huku mshindi wa pili atacheza na mshindi wa

INAENDELEA UKURASA 23

# Stars kusaka pointi tatu kwa Zambia

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya soka ya Tanzania 'Taifa Stars', leo saa 11 kwa saa za nyumbani itashuka Uwanja wa Levy Mwanawasa, Ndola, kuvaana na wenyeji wao Zambia, katika mchezo wa kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2026 katika nchi za Marekani, Canada na Mexico.

Stars inacheza mechi hiyo, ikiwa imetoka kufanya maandalizi yake nchini Indonesia ambapo ilicheza mchezo wa kirafiki dhidi ya timu ya taifa ya nchi hiyo na kutoka suluhu.

Mkurugenzi wa Sheria, Habari na Masoko wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Boniface Wambura, amesema Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Damas Ndumbaro, atawaongoza Watanzania kushangilia timu hiyo leo.

Alisema kikosi kiko vizuri, huku wachezaji ambao awali hawakuwapo nchini Indonesia wakiwa tayari wamejiunga na wenzao.

"Morali iko juu, wachezaji wote walioitwa kwa ajili ya mechi hii wamefika, wale ambao hawakuwa Indonesia na wengine walioongezwa wote wapo.

Na tunatarajia mheshimiwa Waziri ataungana na timu leo (jana) akitokea Dar es Salaam, timu ilipata mapokezi mazuri kutoka kwa balozi wa hapa, Luteni Jenerali Mathew Mtingule," alisema Wambura.

Alisema kumekuwa na mabadiliko ya muda katika mchezo huo, kwani awali ulikuwa uchezwe saa 10:00 jioni kwa saa za Tanzania ambapo ni saa 11:00 kwa Zambia, lakini umesogezwa mbele na sasa mechi itachezwa saa 12:00 jioni, muda ambao kwa Tanzania ni saa 11:00 jioni.

Stars iliyo Kundi E, ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi tatu sawa na Zambia na Niger, lakini inazidiwa kwa tofauti

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >